# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Septemba 20, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580344

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 9



## Babu wa miaka 84 ajiandalia kaburi, alijengea bado yu hai

UKURASA 5

RIPOTI MAALUM

# Hii ndiyo hatari ya kuoana ndugu

**DAKTARI** bingwa anena inavyowapa taabu, mzee wa mila asema ya Kenya yamewakuta...*Endelea Ukurasa wa 4*




Rais Dk. John Pombe Magufuli akiwa na mgeni wake Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye na Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma (kulia), wakipiga kofi kwa furaha baada ya marais hao kufungua jengo la Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma jana. **PICHA: IKULU**

## Maalim atamba kumaliza kazi Pemba

UKURASA 2

## Magufuli, Rais wa Burundi wakubaliana mambo manne

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** SIMBA, BIASHARA HATUMWI MTOTO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM, Rais wa Burundi waingia makubaliano

**Na Gwamaka Alipipi, KIGOMA**

SERIKALI za Tanzania na Burundi, zimeingia makubaliano ya kuendeleza na kukuza biashara na kushirikiana katika sekta ya madini hususani Nickel.

Vilevile, serikali za nchi hizo mbili zimekubaliana kushirikiana katika sekta ya usafirishaji na kuimarisha ulinzi na usalama.

Makubalino hayo yalifanyika jana mkoani Kigoma kati ya Rais John Magufuli na mwenzake wa Burundi, Evarist Ndayishimiye.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya kikao cha ndani, Rais Magufuli alisema wataalamu wa Tanzania na Burundi kutoka nyanja mbalimbali watakutana kufanya mazungumzo kuanza kwa utekelezaji wa makubaliano hayo.

Kwenye sekta ya usafirishaji, Rais Magufuli alisema kutajengwa reli kutoka Uvinza mkoani Kigoma hadi Gitega, Burundi (kilometa 200), itakayosaidia biashara kati ya nchi hizo mbili.

Kuhusu madini, Rais Magufuli alisema wamekubaliana kushirikiana katika uuzaji wa madini ya Nickel kwa wafanyabiashara wa Burundi kuuza madini yao Tanzania.

"Kule Burundi kuna eneo linaitwa Msangati ambako madini ya Nickel yanapatikana, huku Tanzania yanapatikana eneo la Kabanga. Sasa wafanyabiashara wa Burundi wataweza kuja kuuza madini yao Tanzania," alisema.

Rais Magufuli aliwataka wataalamu wa madini kutoka Tanzania na Burundi kukutana na kujadili namna ya utekelezaji wa makubaliano hayo.

Rais wa Burundi, Ndayishimiye, alisema: "Tumefurahi kuona ushirikiano baina ya Tanzania na Burundi ukiendelea tangu enzi za kupigania uhuru, leo tena tumekubaliana kuboresha maendeleo ya kikanda na kimataifa, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni."

Aliongeza kuwa makubaliano waliyoingia yatazidisha ushirikiano wa kindugu ulioasisiwa na waasisi wa nchi hizo mbili hizo.

Alisema ushirikiano ulioingiwa baina ya mataifa hayo mawili kutarahisisha mtiririko wa kibiashara na watu, pia ujenzi wa bandari eneo la Kwara kusaidia usafirishaji wa mizigo.

Awali, wakati wa mapokezi katika Uwanja wa Lake Tanganyika, Rais Ndayishimiye alikaribishwa kwa gwaride na kupigwa mizinga 21 na Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Akizungumza na wananchi waliojitokeza katika uwanja huko, Rais Magufuli alisema Rais Ndayishimiye amekuja Tanzania kwa mazungumzo ya kiserikali.

Alisema kiwango cha ufanyaji biashara Kati ya Tanzania na Burundi kimeongezeka kutoka Sh. bilioni 115.25 mwaka 2016 hadi Sh. bilioni 201 mwaka huu.

Rais Magufuli alisema Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili miradi 16 kutoka Burundi ikiwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 29.42 na imetoa ajira 544. "Kuna kampuni 10 kutoka Tanzania zilizowekeza Burundi ikiwamo Azam, Benki ya CRDB, Interpetrol na zinginezo. Asilimia 95 ya mizigo kutoka Burundi inapitia Bandari ya Dar es Salaam ambako idadi ya mizigo imeongezeka kutoka tani 379,704 miaka ya nyuma hadi 481,081 mwaka jana," alibainisha.

Rais Magufuli aliongeza kuwa, kwenye sekta ya madini, Tanzania na Burundi zinatarajia kushirikiana kwa Burundi kuuza madini yao mkoani Kigoma kwa kutumia masoko yaliyoanzishwa.

"Tuna mpango wa kujenga mtambo wa kuchenjulia madini ya Nickel, mazungumzo yameanza, tunataka nchi hizi mbili ziuze madini na ziingize fedha za kigeni," alisema.

Aliongeza kuwa Tanzania imeweka mkakati wa ujenzi wa reli kutoka Uvinza-Msongati-Kitega ambayo itasaidia usafirishaji wa madini hayo.

Alisema ununuzi wa meli mbili mpya zitakazofanya kazi katika Ziwa Tanganyika, utasaidia wananchi wa Burundi kufanya biashara na wananchi wa Mkoa wa Kigoma.

Rais Ndayishimiye alimpongeza Rais Magufuli kwa kuijenga Tanzania na kubadilisha Mkoa wa Kigoma.

Alisema kwa sasa hali ya usalama Burundi ni tulivu kulinganisha na miaka ya nyuma, utulivu huo ukitokana na kutambua kuwa Watusi na Wahutu ni ndugu na kwamba wazungu ndiyo waliowatenganisha.

UZINDUZI MAHAKAMA

Wakati huohuo, marais hao walipata nafasi ya kuzindua jengo la Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Rais Magufuli akisema mahakama hiyo imejengwa kwa fedha za ndani.

Alisema ujenzi wa mahakama hiyo utapunguza ucheleweshaji wa kesi kwa kuwa awali wananchi wa Mkoa wa Kigoma walilazimika kusafiri hadi Mkoa wa Tabora kufuata huduma ya Mahakama Kuu.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano, serikali imefanikiwa kuwateua majaji 11 kwenda Mahakama Kuu, majaji 11 katika Mahakama ya Rufani na kuajiri mahakimu 39 na kufanya idadi ya mahakimu nchini kufika 938.




Mgombea Mwenza wa Kiti cha Urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akiburudika kwa tunda aina ya tikitimaji, baada ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika eneo la Ziba, jimbo la Manonga, mkoani Tabora jana. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# Maalim Seif atamba kumaliza kazi Pemba

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MGOMBEA urais wa Zanzibar (ACT-Wazalendo), Maalim Seif Sharif Hamad, amekamilisha awamu ya kwanza ya ziara yake ya mikutano ya kampeni katika majimbo ya Visiwa vya Pemba na sasa anaelekeza nguvu zake Unguja.

Awamu hiyo ya kwanza ilisha juzi, akifanya mikutano mitano ukiwamo wa ufunguzi wa kampeni.

Ofisa Habari wa ACT-Wazalendo Zanzibar, Abeid Khamis Bakar, alisema jana kuwa Maalim Seif mbali na kufanya kampeni za majukwaani, alizuru kwenye maeneo ya wananchi na kujionea shughuli zao za kimaisha.

Alisema mgombea wao huyo alitembelea maeneo ya kilimo cha mboga, mwani, wavuvi, wafugaji wa kuku na wafanyabiashara.

"Wananchi wengi walionekana kuvutiwa na kitendo chake hicho cha kutembelea maeneo yao kwa kuwa ni njia ya kuelewa matatizo ya wananchi na kupanga pamoja njia za kuyatatua.

"Maalim Seif aliwaomba wananchi wampigie kura Oktoba 28 na yeye atahakikisha matatizo yanayowakabili anayatua ndani ya miezi sita ya mwanzo ya uongozi wake," Bakari alisema.

Katika taarifa yake, Bakari alisema Maalim Seif amedai kushangazwa na hatua ya serikali ya kujali zaidi mapato kutoka kwa wafanyabiashara, lakini haiwatengenezei mazingira mazuri ya ufanyajibiashara.

Maalim Seif pia alikumbusha umuhimu wa wasimamizi wa uchaguzi kutenda haki katika uchaguzi huo ili kuepusha migogoro itokanayo na uchaguzi.

# 'Watoa huduma za afya wako hatarini'

**Na Romana Mallya**

WAFANYAKAZI wa afya ambao ni kundi lililopo kwenye hatari ya kupata maambukizi kutokana na kutoa huduma kwa wagonjwa, wameitumia Siku ya Usalama wa Wagonjwa Duniani kuongeza ufahamu kuhusu umuhimu wa usalama wao na wagonjwa.

Wakizungumza katika maadhimisho hayo jijini Dar es Salaam juzi, wafanyakazi hao walisema wako kwenye hatari ya kupata maambukizi kutokana na kutoa huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa tofauti.

Mkurugenzi wa Wauguzi wa Aga Khan, Aika Mongi, alitolea mfano ugonjwa wa corona, akibainisha kuwa umeonyesha hatari kubwa zinazowakabili wafanyakazi wa afya duniani kote.

"Wafanyakazi wa afya wanakabiliana na hatari ya kuambukizwa magonjwa kutokana na kuuguza wagonjwa, kufanyiwa ukatili, ajali, unyanyapaa, magonjwa na hata kifo," alisema.

Alisema madhumuni ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni kuongeza ufahamu kuhusu umuhimu wa usalama wa wafanyakazi wa afya na namna wanavyohusiana na usalama wa wagonjwa.

Mkurugenzi huyo alisema wanayatumia maadhimisho hayo kuwashirikisha wabia na kuchukua mbinu za aina mbalimbali ili kuboresha usalama wa wafanyakazi na wagonjwa.

Pia, kutekeleza kwa haraka na kuchukua hatua endelevu ambazo zinatambua na kuwekeza katika usalama wa wafanyakazi wa afya kama jambo la kipaumbele kwa usalama wa wagonjwa na wafanyakazi.

Mkurugenzi wa Tiba wa hospitali hiyo, Dk. Ahmed Jusabani, alisema maadhimisho hayo yamebebwa na kaulimbiu ya 'Usalama wa Wafanyakazi wa Afya: Kipaumbele kwa Usalama wa Wagonjwa'.

Alisema madhumuni makuu ya siku hiyo ni kukuza ufahamu wa kimataifa kuhusu usalama wa wagonjwa, kuongeza ushiriki wa wananchi katika kutibu wagonjwa, kukuza uelewa wa kimataifa na kupunguza madhara.

# Mgombea aahidi ajira milioni 10

**Na Boniface Gideon , TANGA**

MGOMBEA wa Urais kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, amesema endapo atapata ridhaa ya kuwa Rais, atatengeneza zaidi ya ajira milioni 10 kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Akizungumza jana katika mkutano wa kampeni Maramba (Mkinga) na Mashewa wilayani Korogwe, Sendiga alisema mbali na ajira, atatengeneza miundombinu ya barabara.

Pia alisema sekta za kilimo, elimu na afya zitapewa kipaumbele katika uongozi wake sambamba na kukuza sekta ya uvuvi na kujenga viwanda vya usindikaji wa mazao. Alisema maeneo hayo ndiyo yatawezesha kutengenezwa kwa ajira hizo.

Kuhusu hali ya miundombinu ya barabara nchini hususan Mkoa wa Tanga katika wilaya za Korogwe na Mkinga, mgombea huyo alisema atahakikisha anazijenga ili kuziunganisha wilaya hizo pamoja na makao makuu ya mkoa.

Mgombea huyo alisema barabara hiyo itajengwa kwa lami kutoka Maramba hadi Korogwe kupitia Mashewa na Maramba hadi Tanga mjini ili kuinua kiwango cha uchumi wa maeneo hayo.

Kuhusu kilimo, alisema akipatiwa ridhaa hiyo, atahakikisha sekta hiyo inakuwa na tija kwa wakulima kwa kuwa atahimiza matumizi ya teknolojia ya kisasa na wakulima watakuwa huru kuuza mazao yao.

Sambamba na hilo, alisema atahakikisha wananchi wanapata maji safi na salama kwa kwa kutengeneza miundombinu ya maji na kuwataka wananchi wawachague madiwani, wabunge na Rais kupitia chama hicho.



Kiongozi wa chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe ,akihutubia mkutano wa uzinduzi wa kampeni za mgombea ubunge wa jimbo la Lulindi kwa tiketi ya chama hicho, Jerome Bwanausi, wilayani Masasi mkoani Mtwara, jana. **PICHA: SAID POWA**

# Majaliwa: Hakuna kiongozi kama JPM

**Na Mwandishi Wetu, BUTIAMA**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema kati ya wagombea urais waliojitokeza kuwania urais, hakuna kiongozi zaidi ya Dk. John Magufuli.

"Nimekuja kuomba kura kwa ajili ya mgombea urais kwa tiketi ya CCM ili apate miaka mitano mingine kwa sababu hakuna kiongozi bora kati ya wote waliojitokeza zaidi ya Dk. John Pombe Magufuli.

"Wanaokuja kuomba uongozi ni wengi, lakini hakuna chama chenye benki ya viongozi kama CCM. Hakikisheni mnatupatia viongozi wa CCM ili wafanye kazi pamoja na kwa kuelewana," alisema Majaliwa wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Butiama wilayani Butiama mkoani Mara.

Alitumia mikutano yake wilayani hapa kumwombea kura mgombea urais huyo, mgombea ubunge wa Bunda, Boniface Getere, wagombea udiwani wa wilaya zote mbili za Butiama na Bunda. Mgombea ubunge wa Butiama, Jumanne Sagini, amepita bila kupingwa.

Alisema uongozi ni lazima utengeneze timu inayofahamiana na inayozungumza lugha moja, akifafanua: "Chama Cha Mapinduzi kimeleta viongozi watatu safi. Kwa hiyo, ukienda kupiga kura chagua hao watatu ambao ni mgombea urais, ubunge na udiwani.

"CCM inaleta tochi inayowaka na kumulika maeneo ya kuleta maendeleo. Ili iwake na kuleta hayo maendeleo, ninaomba usichanganye betri kwa kuweka gunzi hapo katikati. Je, ukiweka gunzi, hiyo tochi itawaka na kumulikia maendeleo?" Majaliwa alihoji.

Jana asubuhi, Majaliwa alipita nyumbani kwa Baba wa Taifa katika Kijiji cha Mwitongo na kumjulia hali Mama Maria Nyerere.

## Kivuli cha Mwakyembe chamtesa mgombea ubunge

**Na Mwandishi Wetu, Kyela**

MKAKATI wa mgombea ubunge jimbo la Kyela kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Ally Mlaghila, wa kuendelea kujinadi kwenye mikutano ya kampeni bila kuzungumzia miradi iliyotekelezwa na mtangulizi wake, umeanza kukipa faida Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Baadhi ya viongozi, wanachama wa CCM na wananchi wengine waliozungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, walisema mkakati huo unakiondolea chama tawala mtaji na msingi muhimu wa kura.

Walisema hatua hiyo inainufaisha CHADEMA ambayo inaielezea miradi yote kwa ufasaha na kuahidi kuiendeleza huku pia ikibainisha changamoto zilizoko jimboni humu.

Kwa kutambua kazi kubwa iliyofanywa na mbunge aliyemaliza muda wake, Dk. Harrison Mwakyembe, pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, mgombea ubunge wa CHADEMA, Alinanuswe Mwalwage, ameonyesha kuwa kivutio kwa wapigakura.

Katika kampeni zake, Mwalwage amekuwa akikiri kuwa maendeleo hayana chama, hivyo kupongeza kazi iliyofanywa na serikali ya CCM na kuelezea baadhi ya kasoro na kuahidi kuyafanyia kazi.

Hatua hiyo inawafanya baadhi ya wananchi wanaamini kuwa mgombea huyo wa CCM ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama hicho Wilaya ya Kyela, bado anasumbuliwa na mivutano iliyojitokeza kwenye kura za maoni pamoja na kwamba watiania wenzake 39 wametamka hadhani kuwa wanamuunga mkono.

Mlaghila ambaye vikao vya juu vya CCM vilirejesha jina lake kuwania ubunge Kyela, hamtaji kabisa mtangulizi wake wala miradi iliyofanikishwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na kuwaachia CHADEMA uwanja mpana wa kisiasa kujimwaga.

Alidhihirisha hivyo hata siku ya uzinduzi wa kampeni zilizofanyika mjini hapa Septemba 11, mwaka huu, ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Philip Mangula.

Katika uzinduzi huo, Mlaghila hakutaja kabisa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye jimbo hilo miaka mitano iliyopita au kabla.

Akitumia kauli ya Rais Magufuli ya maendeleo hayana chama, mgombea wa CHADEMA, Mwalwage, anaitaja miradi mikubwa iliyotekelezwa kipindi cha nyuma na kusema inaendana na matarajio yake na chama chake katika kutatua kero za wananchi.

Miradi mikubwa iliyotekelezwa kipindi cha nyumba ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Kikusya - Matema (km 39.5), ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha mpakani na Malawi (Kasumulo) na ujenzi wa chelezo katika bandari ya Itungi.

Mingine ni ujenzi wa meli tatu katika Ziwa Nyasa, mradi wa maji wa Kapapa wa unaohudumia wananchi 13,500; Kituo cha Afya cha Ipinda, ukarabati mkubwa Hospitali ya Wilaya na ujenzi wa vituo vya afya vikiwamo vya Njisi na Kilasilo.

# Hii ndiyo hatari kuu ndoa ‘kaka na dada’

## ■Daktari bingwa anena inavyowapa tabu
## ■Mzee wa mila: Ya Kenya, yametukuta




Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Crispin Kahesa.

**Na Romana Mallya**

NI takriban wiki moja sasa, macho, masikio na hisia za umma zilipoelekezwa Kenya katika tukio la kaka na dada kufunga ndoa.

‘Bomu’ lilipasuka kilipofika kipengele cha hatua ya kuvalishana pete, mfungisha ndoa kanisani alipouliza kama kuna pingamizi lolote kama ulivyo utaratibu.

Hapo ndipo mkono wa baba mzazi uliponyooka juu, na alipopewa fursa, ‘hakupepesa macho’, akianika ukweli uliopo kwamba wote hao ni uzao wake huku umma wa cherekochereko ukibaki mdomo wazi kwa staili tofauti.

Katika ufafanuzi wake, Mzee James Sidai alibainisha kwamba, Bwana Harusi, Jonathan Munini, na Bibi Harusi, Ann Magwi, ni wa uzao wa baba mmoja ambaye ni yeye mwenyewe hata ikabidi kuzuia rasmi kufungwa kwa ndoa hiyo.

Kufuatia tukio hilo, chereko, pilau, serebuka na mengine mengi yakaishia hapo na mijadala, minong’ono, kutikisa vichwa na ‘umbea’, vyote vikachukua nafasi yake.

TAFSIRI PANA

Hilo lililoshuhudiwa kwa majirani Kenya huenda ni kati ya mengi yaliyochukua nafasi nchini, lakini simulizi zake hazikwenda mbali kwa sababu ya mwanya wa utandawazi na mawasiliano.

Je, nchini hali ikoje?

Nipashe ilichukua hatua ya kumdadisi Mzee wa Mila, Rocket Mwashinga, aliyekula chumvi kwa miaka 77 ambaye pia ana kofia ya pili ya wadhifa kwa kijamii akiwa Chifu Mkuu wa Mbeya Mjini na Vijijini.

Mzee Mwashinga anakiri katika jamii yake na uzoefu wa kimaisha hilo siyo jambo geni katika mazingira yake, akirejea ushuhuda wa matukio matatu, picha ileile ya kilichotokea kanisani Tana River, Kenya wiki iliyopita.

Anafafanua kuwa, walishakutana na matukio ya ndugu kupendana na kutaka kuoana na wakachukua hatua kama ya kanisani Tana River walipovunja na kupiga marufuku kimila tendo hilo.

“Kuna kijana alikaa kinyumba na mwenzake mkoani Arusha kwa muda wa miezi mitatu na alipokuwa akifanya mchakato wa mahari hapa Mbeya, alibaini binti aliyetaka kumuoa ni mtoto wa baba yake mdogo, hivyo uhusiano huo ulivunjwa kimila,” anasema.

Mzee Mwashinga anaendelea: “Endapo binti angekuwa mjamzito, ingefanyika mila ya kulambishwa dawa maalum ili kukinusuru kiumbe kilichopo tumboni kisizaliwe na matatizo ya kiafya. Haiwezekani ndugu wakaoana, watazaa watoto wenye ulemavu.”

Katika kudhibiti mwelekezo huo, Chifu Mwashinga ana ushauri kwamba vijana wahakikishe kuwa kabla ya kuanza uhusiano, wachunguzane kwanza ili kujua historia ya familia zao endapo ni ndugu.

Hata hivyo, katika baadhi ya jamii nchini na hata maeneo mengine duniani, likiwamo Bara Asia, ndoa za undugu katika jozi kama: Kaka na dada; mtoto wa baba mdogo na baba mkubwa; mjomba na shangazi; ni ruksa, tena zinazoshuhudiwa na chereko za babu, bibi ndugu na jamaa.

Vilevile, yanayojiri katika mwenendo wa kiutandawazi, sasa limekuwa jambo la kawaida, vijana kuchumbiana wakiwa wamekutana katika maeneo ya mbali ndani ya nchi au nje ya mipaka ya nchi na baada ya safari ndefu huenda kukawapo mtoto au watoto na mali za pamoja kisha kunafanyika hatua ya kwenda kujitambulisha nyumbani.

**WATAALAMU WA AFYA**

Dk. Crispin Kahesa, ni mtaalamu bingwa anayepatikana katika Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) jijini Dar es Salaam, ana maoni kadhaa kwa athari zinazopatikana kwa ndoa zenye jozi ya aina hiyo.

Hivyo, Dk. Kahesa ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Kinga katika taasisi hiyo, anataja njia kuu mbili za madhara ni kuendeleza vinasaba vyenye matatizo kiafya au kimwili na kurithishana magonjwa.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, magonjwa kama kisukari, selimundu, saratani, maradhi ya akili na ualbino, huendelezwa katika kizazi cha ndoa za aina hiyo tajwa.

Katika tafsiri yake ya kitaalamu, anawarejea ndugu walio wazaliwa wa tumbo moja, ndiyo hatari ya madhara ya moja kwa moja.

Shida kuu ni nini? Dk. Kahesa anafafanua: “Sababu kubwa ni vinasaba kuvurugika mpangilio wake, unakuta kinasaba kinachotengeneza chembe hai kinahama kutoka kizazi kimoja kwenda kingine.

“Hatari iko wapi ndugu wakioana? Kama mmetoka kwenye familia moja, kwa kawaida vinasaba vinatokana na chembe hai mbili ambazo unaweza kukuta moja imeathirika na nyingine haijaathirika. Ili ugonjwa utokee, lazima chembe hai zote mbili zionekane na ugonjwa.

“Mara nyingi chembe hai hizi zinabebwa kwenye mayai ya mama au mbegu za baba, ili mtoto atengenezwe kuna muunganiko wa chembe hai kutoka kwa baba na kwa mama.

“Inapotokea mtu mwenye chembe hai moja yenye ugonjwa na nyingine iliyo salama na mwingine ana chembe hai moja salama na nyingine yenye ugonjwa, watu hawa wanapooana, yapo matokeo mengi yanaweza kutokea.

“Cha kwanza, zinaweza kutoka chembe hai zote salama na mtoto atakayezaliwa akawa hana ugonjwa wala hajaubeba, inapotoka chembe hai salama na ikaungana na yenye ugonjwa, usiuone ugonjwa, lakini akawa ameubeba.”

Dk. Kahesa anataja uwezekano wa chembe hai za pande mbili zenye ugonjwa zikaungana na tatizo likajitokeza kwa mtoto wako moja kwa moja, hivyo familia kuwa na historia ya kuwa na magonjwa ya kurithi kama saratani, kisukari, selimundu, ualbino au ugonjwa wa akili.

Ushauri wa daktari huyo ni kwamba kunapaswa kuchukuliwa tahadhari ya kutooana ndugu ili kutoendeleza magonjwa waliyonayona pia wanajamii hao wana wajibu wa kupata ushauri wa kitaalamu na kuchukuliwa vipimo kwa mtazamo wa kudhibiti athari za kiafya.

Dk. Kahesa anasema huduma hiyo ya vipimo na ushauri kwa sasa inapatikana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) yenye maabara ya kupima vinasaba ili kugundua aina ya magonjwa ambayo familia imebeba na kupewa ushauri.

Anatoa mfano kwa ugonjwa wa selimundu, kwamba kinachopaswa kiafya ni kufunga ndoa na mtu wa jamii ya mbali ambaye pia kiafya yuko mbali na uwezekano wa maradhi hayo.

Vilevile, anasema wagonjwa wa saratani wakiwa na umri wa chini ya miaka 25, wengi wao uzoefu unaonyesha kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kurithi.

Abainisha kuwa takwimu zinaonyesha asilimia tano ya wagonjwa wa saratani wanaangukia kwenye kundi hilo, akishauri “mtu akitaka kuoa, ni vyema aoe familia za mbali,” alisema.

***USIKOSE WIKI IJAYO MWENDELEZO WA MAZITO YA NDOA ZA KAKA NA DADA**

MAKALA




Mkazi wa Kijiji cha Mahanje, Kata ya Kwafungo, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Stephano Philipo Joseph (84), akionyesha kaburi alilolichimba na kulijenga vizuri lenye thamani ya Sh. Milioni 7 kwaajili yake siku atakapokufa, kwa madai kuwa hana ndugu na watoto wake wamemtenga baada ya kutengana na mke wake mdogo aliyemtaja kwa jina la Penzia Martine. Makaburi mengine yanayoonekana ni ya watoto wake waliokwishafariki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Babu achimba kaburi lake na kulijengea akiwa bado yu hai

**Aliwataja watoto aliozaa na mke wake huyo kuwa ni Faustine, Alphoncia, Luvina, Isdory na mwingine aliyefariki dunia bado mchanga. Baadhi ya watoto wake hao walishafariki dunia na wamezikwa katika eneo ambalo amechimba kaburi lake.**

**Na Steven William, MUHEZA**

KUISHI ni kuona mengi. Hii ndiyo hali halisi ya maisha ya kila siku ya mwanadamu kwani kila uchao jambo jipya huibuka. Yako mambo ya kushangaza, kuchekesha na hata kuhuzunisha.

Kwa maana nyingine, maisha yamejaa kila aina ya mambo na vitu ambavyo kama mtu hajalia basi atacheka. Kama hajalia au kucheka, basi atashangaa.

Hivyo ndivyo ilivyotokea huku Mahanje, Kata ya Kwafungo, Muheza mkoani Tanga, baada ya Mzee Stephano Mwinuka kutoa kali ya mwaka baada ya kujichimbia kaburi ambamo atazikwa na kulijengea kabisa.

Jambo kama hilo ni kama vile uchuro kwa baadhi ya makabila lakini kwa Mzee mwinuka (84) limekuwa la kawaida kwani ameamua kufanya hivyo akiwa hai. Mbali na kulichimba, ameamua kulijengea kabisa na kuweka marumaru.

Hatua ya Mzee Mwinuka kufanya hivyo, imewashangaza wengi wilayani Muheza ambao wamefanya sehemu hiyo kuwa kama kivutio cha utalii kutokana na watu wa maeneo mbalimbali kufunga safari kwenda kushuhudia kaburi hilo.

Mwinuka, ambaye kabila lake ni Mpangwa wa asili ya Ludewa mkoani Njombe, anasema ameamua kujichimbia kaburi hilo kwa gharama kubwa akiwa hai akidai ni maandalizi ya kutayarisha nyumba yake ya milele ili akifa asipate taabu ya kuhangaisha watu kuchimba kaburi.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii katikati ya wiki kijijini hapo, Mwinuka alisema alihamia Muheza mwaka 1956 akitokea kijiji cha Lugalawa, wilayani Ludewa.

Mwinuka alisema alihamia kijijini hapo mwaka 1960 na kuanza kujishughulisha na kilimo cha mahindi, machungwa, minazi, mananasi na miwa katika shamba lake la zaidi ya ekari 50.

Alisema alifika kijijini hapo akiwa na mke wake, Hilalia Hilary, aliyezaa naye watano lakini ameshatangulia mbele za haki.

Aliwataja watoto aliozaa na mke wake huyo kuwa ni Faustine, Alphoncia, Luvina, Isdory na mwingine aliyefariki dunia bado mchanga. Baadhi ya watoto wake hao walishafariki dunia na wamezikwa katika eneo ambalo amechimba kaburi lake.

Baada ya kufa mke wake wa kwanza, alisema alioa mke mwingine aliyemtaja kwa jina la Penzia Martine ambaye waliishi pamoja kwa nae kwa muda mrefu na kuzaa naye watoto wanne.

**Sababu nyingine ya kuchimba na kujenga kaburi hilo ni apumzishwe baada ya kufa kwa kuwa ana hofu ya kutupwa kama mnyama kutokana na watoto wake kumtupa na pia hana hata ndugu si Muheza wala Tanga.**

Stephano aliwataja majina ya watoto aliozaa na mke mdogo kuwa ni Anastazia, Teresia, Regina na Joseph ambapo wengine wamefariki dunia na wengine wako hai.

Alisema baada ya hapo walitengana na mke huyo ambaye alikimbia nyumba waliyokuwa wanaishi na hatimaye kumwacha mume wake yapata miaka 20 sasa.

Mzee huyo alisema mwanamke huyo aliwashawishi watoto nao waondoke katika nyumba hiyo na wasiwe na uhusiano kabisa na baba yao na wasifike hata kumsalimia.

Baada ya kuona hali hiyo na watoto wake hawamjali baada ya kushikiwa akili na mama yao, alisema alianza kuishi peke yake na kupata shida kama vile hajazaa mtoto yeyote.

Mwinuka alisema baada ya kuona hali hiyo na katika kijiji hicho hana ndugu kwa kuwa aliwaacha Ludewa, na wengine hawajui kabisa, aliamua kuchimba kaburi kabisa la kuzikwa wakati bado mzima ili asisumbue watu pindi atakapofariki dunia.

Kwa mujibu wa Mwinuka, baada ya kuchimba kaburi hilo, aliamua kutumia fedha nyingi kulijengea kwa marumaru ndani na nje pamoja na kifuniko chake ili lisididimie pindi mvua itakaponyesha. Pia ameweka msalaba juu ya kaburi hilo pamoja na kuweka picha yake huku akijenga kibanda kikubwa chenye mlango na ameweka kufuri ili watu wasiingie ndani.

Sababu nyingine ya kuchimba na kujenga kaburi hilo ni apumzishwe baada ya kufa kwa kuwa ana hofu ya kutupwa kama mnyama kutokana na watoto wake kumtupa na pia hana hata ndugu si Muheza wala Tanga.

**MAANDALIZI ZAIDI**

Licha ya kujenga kaburi na kulitia nakshi, pia alisema tayari ameshafanya maandalizi makubwa pindi kifo chake kitakapotokea ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kununua mchele na ng'ombe na mbuzi ili watu wale na kushiba baada ya kuzikwa.

Licha ya maandalizi hayo, pia alisema ameanza kuuza sehemu ya shamba lake ili fedha anayoipata aanze kuitumia kabla ya kufa.

Aliyekuwa Diwani wa Kwafungo, Gabriel Mswagala, ambae anagombea tena nafasi hiyo, alisema kitendo hicho kimewashangaza watu wengi.

Mswagala alisema hali hiyo imesababisha watu kwenda kijijini hapo kuangalia kaburi hilo na sasa sehemu hiyo imekuwa kama sehemu ya kutalii huku wengine wakisema huo ni uchimvi mkubwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tabia hizi katika uchaguzi zikemewe kwa nguvu zote

**TANGU** kuanza kwa kampeni kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu, kumejitokeza mambo mbalimbali kinyume cha sheria na kanuni za mchakato huo.

Katika siku za awali, Watanzania walishuhudia vijembe vikitawala baina ya wagombea wa vyama vinavyoshiriki uchaguzi huo, huku matusi nayo yakitamalaki. Kutokana na hali hiyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliibuka na kukemea huku ikitishia kuwachukulia hatua watakaoendeleza vitendo hivyo.

Pamoja na kuwapo kwa vitendo hivyo, vyama vya siasa, vikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinachoomba ridhaa tena ya kuongoza na kile kikuu cha upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kila kimoja kililalamika kuwa kinafanyiwa nchezo huo usio wa kistaarabu katika medani za siasa.

Lakini kama vile haitoshi, kumeibuka malalamiko mengine na safari hii kutoka kwa CCM kudai kuwa kuna makundi ya watu, wapinzani wakituhumiwa, kuwa wanaharibu mabango yao zikiwamo picha za wagombea wake wa urais na ubunge.

Malalamiko hayo yalitolewa hivi karibuni na chama hicho Mkoa wa Shinyanga, wakati wa uzinduzi wa kampeni zake kimkoa uliofanyika mjini Kahama huku kikiweka wazi kuwa wanaofanya hivyo ni wafuasi wa vyama vya upinzani ambao wamechana baadhi ya picha za mgombea wake wa urais, Rais John Magufuli.

Kutokana na kuibuka kwa tabia hiyo, chama hicho kilisema kimejipanga kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani watakaokamatwa kwa kuhusika na vitendo hivyo.

Katika taarifa yake, uongozi wa chama katika mkoa huo uliweka wazi kwamba vitendo hivyo sivya kistaarabu. Viongozi hao walikwenda mbali zaidi wakisema vitendo kama hivyo vikiwamo vya kutupiana mawe na kuvunjiana vioo vya magari vinapaswa kukemewa na wapenda amani kote nchini.

Ni ukweli kwamba tabia kama hizo hazipaswi kuendelea kuendekezwa kwa sababu Tanzania tangu kupatikana kwa uhuru, haijawahi kumwaga damu. Kama vitendo hivyo vitaachwa viendelee, ni wazi kwamba tunaweza kushuhudia uvunjifu wa amani na kutia doa uchaguzi mkuu.

Licha ya kwamba CCM ndiyo iliyolalamika kufanyiwa hivyo, inawezekana pia katika baadhi ya maeneo vyama vingine pia vimefanyiwa vitendo kama hivyo.

Kwa ujumla, vitendo hivyo vimepitwa na wakati na havipaswi kufanywa na Watanzania ambao wamekuwa wakiimba amani, umoja na mshikamano bila kujali itikadi zao za kisiasa wala imani zao za kidini.

Ni vyema kila chama kikanadi sera zake kupitia ilani yake ya uchaguzi ili kuwashawishi wananchi wawachague itakapofika siku ya kutekeleza haki yao ya kidemokrasia. Vyama vinavyoendekeza tabia za vurugu na kuharibu picha na mabango ya vyama vingine, vitambue kuwa huo si ustaarabu wa Kitanzania bali ni tabia zisizo za kiutu.

Vitendo kama hivyo vinapaswa kukemewa na wapenda amani kote huku vyombo vilivyopewa dhamana ya kuhakikisha uilinzi na usalama unadumishwa, vichukue hatua zinazostahili dhidi ya watu wanaofanya hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kamatakamata hii ya magari inaashiria vitendo vya rushwa

Na Mwandishi Wetu

JESHI la Polisi limepewa dhamana ya kusimamia usalama wa raia na mali zao ikiwamo kudhibiti vitendo vinavyoweza kuhatarisha uhai wa binadamu na uvunjifu wa amani.

Kutokana na wajibu huo, jeshi hilo limekuwa likifanya kila njia kuhakikisha Watanzania wanaishi kwa amani na utulivu.

Katika kuhakikisha hilo linatekelezwa, kumekuwa na jitihada za kupambana na majambazi pamoja na wahalifu wadogo, maarufu kama vibaka.

Aidha, katika kudhibiti madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani, polisi kupitia kikosi chake cha usalama barabarani, kimekuwa kikiwachukulia hatua wale wote wanaokwenda kinyume.

Miongoni mwa adhabu zinazotolewa ni pamoja na kuwatoza faini wakiukaji na wale waliopitiliza wakifikishwa katika vyombo vya sheria na hata kunyang'anywa leseni zao.

Pamoja na kazi hiyo nzuri inayofanywa na askari hao kwa kusimamia sheria, kuna jambo moja ambalo limekuwa sawa na donda ndugu na linalotia doa jeshi hilo miaka nenda miaka rudi. Jambo hilo si lingine bali ni rushwa, vitendo ambavyo vinaendekezwa na askari wachache.

Baada ya kukithiri kwa rushwa ndani ya jeshi hilo, huku washukiwa na watuhumiwa wakuu wakiwamo askari wa usalama barabarani na wale wa doria, maarufu kama Tigo, viongozi wa sasa na wale waliopita ndani ya jeshi walijitokeza mara kwa mara na kukemea vikali.

Hatua hiyo ya kukemea iliyofanywa na viongozi hao akiwamo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, na aliyekuwa mtangulizi wake, Kangi Lugola, kwa kiasi fulani tabia hiyo ilipungua.

Kupungua kwa vitendo hivyo pia kulitokana na kukua kwa teknolojia hasa mitandao ya kijamii ambayo ilishiriki kwa kiasi kikubwa kuwaanika wanaojihusisha na tabia hiyo.

Pamoja na kazi hiyo nzuri inayofanywa na askari hao kwa kusimamia sheria, kuna jambo moja ambalo limekuwa sawa na donda ndugu na linalotia doa jeshi hilo miaka nenda miaka rudi. Jambo hilo si lingine bali ni rushwa, vitendo ambavyo vinaendekezwa na askari wachache.

Lakini kama wahenga wasemavyo ni vigumu mtu aliyezoea wizi kubadili tabia, ndivyo ilivyojitokeza kwa baadhi ya askari kuanza tena kuomba na kupokea rushwa na mbinu kubwa wanayotumia ni kuwabambikia makosa baadhi ya madereva wa magari ya abiria na yale binafsi.

Licha ya kufanya hivyo, baadhi ya askari hao wamebadili mbinu kwa kuwavizia waendesha vyombo vya moto kwenye barabara za vichochoroni ambako magari machache yanapita.

Jambo hilo limekithiri na linazidi kushika kasi katika jiji la Dar es Salaam. Baadhi ya askari hao wamekuwa wakienda na kujificha katika barabara za pembezoni na kusimamisha magari yanayopita maeneo hayo.

Mfano ni barabara ya Kisukulu ambako wamekuwa wakitumia magari binafsi na kujificha chini ya miti huku wakivizia magari yanayopita na kuyasimamisha.

Vitendo kama hivyo katika barabara hiyo hasa eneo la Bosnia na Kwa Swai kuelekea Kimanga, vilikoma baada ya kutokea tafrani kati ya askari hao na ofisa mmoja wa serikali waliyemkamata na kumpiga huku wahusika wakuu wakiwa askari waliokuwa wakivizia pikipiki, magari binafsi na yake madogo ya kubeba mizigo, maarufu kama Kirikuu.

Ni muhimu viongozi wa polisi chini ya Mkuu wa Jeshi hilo, Inspekta Jenerali Simon Sirro, wakatambua kwamba vijana wao 'wamebadili gia angani' katika kuendeleza tabia ya kuomba na kupokea rushwa.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Kwa wenzetu kulipa kodi ni sawa na kifo haiepukiki



**Na Nkwazi Mhango**

BAADA ya Serikali ya Rais John Magufuli kubana matumizi na kuimarisha ukusanyaji kodi, huwa napata malalamiko ya baadhi ya marafiki zangu kuhusu kodi. Huwa nashangaa ikizingatiwa kuwa mazuri yote ambayo nchi yetu imeyafanya na kuyafikia haraka yangekuwa ndoto kama ukusanyaji kodi usingefanyika vilivyo.

Hata hivyo, sishangai sana. Malalamiko hutokana na ukweli kuwa wengi hawakuwa wamezoea kulipa kodi vilivyo hima kutokana na mfumo wa kijamaa tulioanza nao au kutojua umuhimu wa kufanya hivyo kwa faida ya nchi na wananchi wake.

Sababu nyingine ni uzembe wa kuhimiza kukusanya kodi. Hapa Kanada, kulipa kodi ni sehemu ya ustaarabu na utaratibu wa kawaida. Si kulipa kodi tu bali hata kujaza taarifa za mwaka za kodi kwa kila mwananchi na mkazi ambaye si mwananchi wa hapa. Kulipa kodi hapa kunafanyika kwa njia ya kukatwa pesa moja kwa moja toka kwenye kila unachonunua. Ukiingia dukani, utakuta bei ya kila kitu imeandikwa. Kama maandishi yanasema bei ni kiasi fulani, ukikubali kulipa, utaongezewa kodi ya serikali. Hivyo, bei huongezeka tofauti na ile iliyoandikwa.

Kitu kingine, kila unapolipia manunuzi lazima upewe risiti tena siyo lazima uiombe. Hata usipopewa, kwa wale wasiotaka kudai baadhi ya fedha zirejeshwazo kwenye manunuzi yao, muuzaji huchapisha ile risiti na kuitupa kwenye jalala. Lazima ichapishwe kwenye mashine ya manunuzi ya kielektoniki (EFD).

Hapa kila kipato lazima kitozwe kodi bila kujali ukubwa hata udogo wake. Wanaofanya biashara ya kuuza miili yao, watoa simu za biashara hiyo, wanaocheza utupu, watengeneza matoi ya ngono, waendeshaji klabu za maonyesho ya utupu na waigizaji ngono, hawa wanatozwa kodi kama watu waliojiajiri. Wanaouza miili yao hata kama anafanya hivyo kinyume cha sheria anapaswa kutoza kodi na kuhakikisha anatoa risiti ili mteja aamue mwenyewe (kwa wanaotaka kurejeshewa fedha za manunuzi au kutunza kumbukumbu).

David Rotfleisch wa kampuni ya Rotfleisch & Samulovitch P.C anasema kuwa anayeuza mwili huruhusiwa kudai baadhi ya marejesho ya kodi yatokanayo na maandilizi ya biashara kama vile matangazo, vitendea kazi na kadhalika.

Japo biashara hiyo haiwezi kuruhusiwa Bongo, kutokana na kukinzana na maadili yetu, hata ikiruhusiwa, wanaodai risiti watakuwa wachache au wasiwepo.

Wanaofanya biashara hiyo watapenda pesa yao isikatwe kodi. Wateja watagwaya kudai risiti. Maana, baadhi ya maduka huku huchukua taarifa za mteja kama vile anwani, nambari za simu hata baruapepe. Hivyo, wasingependa taarifa zao zijulikane.

Muhimu ni kuelewa: kulipa kodi ni wajibu si wa raia tu bali hata mkazi wa nchi yoyote. Kwa Tanzania ambapo wageni inakuwa vigumu kuwapata kama hakuna utaratibu wa kukata kodi moja kwa moja kwenye bidhaa na huduma anzisheni utaratibu wa kutoza kodi kwenye bidhaa badala ya kuhimiza watu binafsi walipe kodi.

**Sababu nyingine ni uzembe wa kuhimiza kukusanya kodi. Hapa Kanada, kulipa kodi ni sehemu ya ustaarabu na utaratibu wa kawaida. Si kulipa kodi tu bali hata kujaza taarifa za mwaka za kodi kwa kila mwananchi na mkazi ambaye si mwananchi wa hapa. Kulipa kodi hapa kunafanyika kwa njia ya kukatwa pesa moja kwa moja toka kwenye kila unachonunua. Ukiingia dukani, utakuta bei ya kila kitu imeandikwa. Kama maandishi yanasema bei ni kiasi fulani, ukikubali kulipa, utaongezewa kodi ya serikali. Hivyo, bei huongezeka tofauti na ile iliyoandikwa.**

Eneo jingine ambalo lazima mhusika alipe au kusamehewa kodi ni kuhusiana na kutoa huduma fulani kwa jamii au kutoa zawadi. Ukitoa huduma kwa jamii, serikali inakupunguzia kodi. Ila ukitoa zawadi au kununua kitu ambacho si muhimu au cha anasa kama sigara au pombe na magari na matoi ya bei mbaya, kodi huwa kubwa kweli kweli. Mfano hapa ninapoishi, kopo moja la bia yenye ujazo wa juu kidogo ya nusu lita inauzwa zaidi ya dola 3.5 za hapa ambazo ni sawa na takribani shilingi za Kitanzania 7,000 na ushei kutegemeana na kupanda na kushuka kwa shilingi yetu.

Kulipa kodi, licha ya kuwa wajibu wa mwananchi, hutuhakikishia huduma za pamoja toka serikalini. Unapolipa kodi, una haki ya kudai huduma za pamoja kama elimu, ulinzi, miundombinu na mengine kama hayo toka serikalini. Ndiyo maana Rais John Pombe Magufuli amekuwa akiwaambia Watanzania kuwa miradi mikubwa mikubwa aliyofanikisha, imefanikishwa na Watanzania wenyewe kupitia kodi zao. Hivyo, kwa mtu yeyote anayetaka maendeleo katika nchi yake, lazima alipe kodi bila kushurutishwa. Wamarekani wanao usemi kuwa vitu viwili haviepukiki kwa binadamu yaani kifo na kulipa kodi.

### MADONGO YA MGAGAGIGIKO

# Ahadi tamutamu za kampeni!



**Na Joseph Kulangwa**

JUZIJUZI hapa, niko mahali nimechanganyika na watu, wala sijui wanatoka wapi, lakini nikaamini tu sote ni Watanzania na tunajadili mustakabali wa maisha yetu, hasa katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

Niliwasikiliza, mara nikajikuta nakurupuka na kuropoka, eti heri kusiwe na mfumo wa vyama vingi vya siasa! Kwa kweli sikujua kwa nini yalinitoka hayo? Eti nikimaanisha heri turudi kwenye mfumo wa chama kimoja.

Nilipojitambua sikutaka kusahihisha, kumbe nisikilize nitapokewaje hata kama nimefanya kosa, kwa kuwa kundi lile la watu haiwezekani wote waniunge mkono kwa kauli hii yenye ukakasi kwa wengine.

Lakini palipo na wengi pana mengi, wapo walioniunga mkono ingawa kimya kimya. Lakini wasiovumilia nao wakawapo. Akaibuka mmoja akahanikiza, "unasema nini wewe bwege?" Huku kanitolea macho na mate yakimruka, nikashukuru tu kuwa Kovidi alishajiendea kwa maombi ya Watanzania.

Nilipomtazama nikaona bado ananikodolea macho ananiambia "we bwege sema unasemaje, hebu rudia?" Nikaona sasa kama ni bhita basi na iwe mura. Nikajikuta narudia viiile vile, "bora vyama vingi vifutwe!" Nikamsikia anasema "hii mijisisiemu mibwege sana".

Kama akaonekana anashindwa bhita vile, nami nikapata nguvu huku nikiungwa mkono na wachache kweli kweli, tofauti na wale waliomwambia marehemu shemeji yangu Francis Nyalali, kwamba walitaka kuendelea na chama kimoja miaka ile ya tisini.

Nilipopata nguvu, nikaona kama mbwai na iwe mbwai, nikataka sasa nifafanue kile ambacho sasa ni vema nikihalalishe tu, kuwa ndio msimamo wangu pale, nikichelea kuubadii nisijeonekana popo au kinyonga.

Nikawaambia "hivi mnadhani mimi bwege kama alivyosema huyo mjinga wenu hapo? Nina hoja. Hivi si mnaona kampeni zilivyopamba moto, tunatafuta Rais, wabunge na madiwani, halafu mtu tu anaibuka na kuja na miahadi ambayo haiwezi kutekelezwa!

"Hivi hizi nyomi mnazoziona hapa, kuna mtu anaweza kupika ubwabwa na kuku akaja kugawia watu waliofurika uwanjani mathalan pale Zakhem, Kirumba, Kambarage na kwingineko huko? Semeni ukweli kama si hadhaa za kisiasa?

"Tuwe wakweli, hivi mnakubali mtu anasimama hapa anasema mkimpa nji atahamishia bahari Dodoma, kweli? Eti atajenga mitaro ya maji yatoke Bahari ya India hadi Dodoma kweli? Halafu mnakubali kabisa kuambiwa kuwa mkimpa nji atajenga daraja kutoka Dar es Salaam mpaka Zanzibar, eti kwa kuwa mnatapika sana kwenye boti za Bakhressa?"

**"Tuwe wakweli, hivi mnakubali mtu anasimama hapa anasema mkimpa nji atahamishia bahari Dodoma, kweli? Eti atajenga mitaro ya maji yatoke Bahari ya India hadi Dodoma kweli? Halafu mnakubali kabisa kuambiwa kuwa mkimpa nji atajenga daraja kutoka Dar es Salaam mpaka Zanzibar, eti kwa kuwa mnatapika sana kwenye boti za Bakhressa?"**

Yule jamaa yangu nikaona kama anataka kunisogelea anibatue kibao, sikubabaika akaishia kuniuliza, "unamaanisha nani sasa?" Nikamjibu kwa upole "ndugu yangu sikuja hapa kutaja majina, kama wewe hujasikia hayo jikalie kimya, kwani wewe msemaji wao?"

Alipotulia nikaendelea, "humjasikia mtu anasema mkimpa ubunge eti atashona pazia la kuzunguka Mlima Kilimanjaro ili Kenya wasiuone?" He, nikaona wanaangua kicheko hata adui yangu naye sasa ndiye anafuta machozi ya kicheko kwa ukosi wa shati lake chafuuu. Nikashangaa!

Nikamchokoza nikamwuliza; "eti braza wewe hujasikia hayo?" Akanigeuka akanijibu, "achana na mimi!" Mwanzo sikuamini, lakini baadaye nikaamini kuwa kumbe napambana na mvuta msuba. Lakini waliokuwa karibu naye wakanielewa.

Akajitokeza mwingine ambaye niliona kama ananielewa, akasema, "aah we jamaa achana na siasa hizi, watu wanatafuta kula tu humo, wala hakuna kitu, hizo wanaomba kura za kula tu, hawatafanya hayo wanayosema. Ahadi ngapi hapa tunapewa kila miaka mitano lakini zinayeyuka? Tulishageuzwa mabozi tu."

He, mara kusanyiko lile likageuka la siasa kabisa kabisa, watu wakajadili mambo ya siasa, waliosema makali wakawa wanaonyana pale pale. "Ohoo shauri yako mbu kibao wapo hapa we ropoka tu". Ghafla yule adui yangu akanishika mkono na kuniweka pembeni na kuniambia, " mh lakini mshikaji umetufumbua macho na masikio unajua!"

Eti akaniambia naye anatoka katika moja ya vyama vile ambavyo havikusimamisha mgombea urais, bali vinashangilia mgombea wa chama kingine, huku wakiomba huruma ya kuachiwa angalau wabunge. Akaniambia, "bora turudi tu kule tulikokuwa kabla ya 1992". Sikumwamini nikasepa zangu.

## KONA YA UKWELI

# Vyama vya siasa haviwezi kujengwa kwa ruzuku pekee



Na Thobias Mwanakatwe

SERIKALI ilipoamua kuurejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, baada ya kuufuta mwaka 1965, moja ya utaratibu ulioelezwa ni vyama hivyo kupewa ruzuku ya kuviwezesha kuendesha shughuli zao.

Pamoja na kwamba Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya mwaka 1992, vyama vya siasa havikupewa ruzuku hadi baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 ambao ulikuwa ni wa kwanza tangu Tanzania ilipoingia katika mfumo huo wa kisiasa.

Baada ya uchaguzi huo, utaratibu wa kutoa ruzuku ulibadilishwa tena mwaka 1996 na sheria ilitaka vyama vinavyopewa ruzuku viwe vimepata zaidi ya asilimia tano ya kura katika uchaguzi mkuu.

Kigezo kingine kilichowekwa na serikali ni kwamba chama husika hakina budi kuwa na wabunge. Hata hivyo, hakuna maelezo yaliyotolewa kuhusiana na vyama kuwa na sifa hizo lakini kwa kiasi kikubwa sababu za kutaka vyama vitimize sifa hizo ni kutaka kuwapo na vyama makini vya siasa nchini na si vyama vya ruzuku.

Naamini kuwa serikali ililazimika kuweka vigezo hivyo kutokana na uzoefu ilioupata mwaka 1995 ilipotoa ruzuku kwa vyama vyote vilivyokuwa vimepata usajili wa kudumu kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi mkuu.

Nakubaliana kabisa kwa asilimia 100 na uamuzi huo wa serikali wa kuweka vigezo hivyo kwani ni jambo lililo wazi kuwa licha ya kwamba Tanzania tuna zaidi ya vyama 17 vyenye usajili wa kudumu, vingi vipo kama havipo.

**Utashangaa hata katika kipindi hiki baadhi ya wagombea urais wamekuwa wakilalama tu kwamba vyama vyao vinakabiliwa na ukata lakini unajiuliza kwa nini haviwi na mikakati ya kupata fedha ikiwamo kuanzisha miradi itakayoviingizia kipato badala ya kulilia ruzuku.**

Baadhi ya vyama vimekuwa vikiibuka kama uyoga unapofikia wakati wa uchaguzi mkuu pengine vinafanya hivyo ili kupata ufadhili wa kifedha kutoka kwa washirika wao wa ndani na nje.

Baada ya uchaguzi kwisha, vyama hivyo vinapotea kabisa kiasi kwamba Watanzania wengi wanaviona kama ni vyama vya msimu kwa lengo la kutaka kupata ruzuku ambayo inatolewa kwa vyama vilivyotimiza masharti hayo.

Utashangaa hata katika kipindi hiki baadhi ya wagombea urais wamekuwa wakilalama tu kwamba vyama vyao vinakabiliwa na ukata lakini unajiuliza kwa nini haviwi na mikakati ya kupata fedha ikiwamo kuanzisha miradi itakayoviingizia kipato badala ya kulilia ruzuku.

Na bahati mbaya hata baadhi ya vinavyopata ruzuku vimekuwa na matumizi yasiyoridhisha. Tumekuwa tukishuhudia kila mwaka, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akiviumbua kutoka na matumizi yasiyoridhisha ya fedha hizo za ruzuku.

Inashangaza kuona baadhi ya vyama licha ya ukongwe wake vinashindwa hata kujenga ofisi zake za kudumu na badala yake vinapangisha lakini vinapata ruzuku jambo ambalo ni fedheha kwa vyama hivyo.

Ufike wakati Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo ndiyo inavilea vyama hivyo, itunge sheria ambayo italazimika kuvifuta vyama ambavyo haviko 'active' ili kuondokana na msululu wa vyama ambavyo havina faida na uwepo wake.

Hatuwezi kuwa na vyama vya siasa ambavyo havifanyi siasa badala yake vinavizia tu inapofika wakati wa uchaguzi mkuu ndipo vinaibuka kama uyoga na kuja na ilani zenye mambo mengi ambayo hata vikipewa madaraka haviwezi kuyatekeleza.

Vyama vinavyoibuka wakati wa uchaguzi tu ndivyo ambavyo vinakuja kuwachanganya wananchi kwa kutoa sera ambazo vinatambua ni ngumu kutekelezeka.

Japokuwa kunaweza kukawa na hoja kwamba miaka mitano ya utawala huu havikuruhusiwa kufanya siasa, lakini hiyo si kweli siasa ingeweza kufanyika kwa kupitia kwa viongozi wao ambao ni wabunge na kadhalika.

Umefika wakati sasa vyama vya siasa viache kufikiria na kudhani kuwa haviwezi kuishi kuendelea na majukumu yake bila kupata ruzuku inayotolewa na Serikali.

*KWA MAONI NA USHAURI TUWASILIANE*

*mwanakatwe2015@gmail.com*

## DARASA LA NDOA....

# Usiri, ubinafsi ni sumu katika ndoa



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka 0744000066.

SUALA la fedha limeathiri ndoa nyingi na hata zingine kusambaratika. Baadhi zinapumulia mashine na zingine zipo kama hazipo. Yote hiyo ni kwa sababu ya fedha.

Fedha inapotumika visivyo inaweza kuleta madhara makubwa ndani ya ndoa. Lakini ikitumika vizuri, inakuwa baraka kubwa kwa wanandoa.

Kutokana na ukweli huo, suala la fedha linapaswa kuwekewa msingi mzuri kwa watoto kwa maana ya kufundishwa thamani na nidhamu ya fedha. Watoto wasipewe fedha nyingi za kutumia shuleni kila siku.

Pia wanapaswa kufundishwa kuwa si wakati wote wanaweza kupata wanachotaka. Kadri wanavyokua, waelekezwe kuwa na nidhamu ya fedha kwani leo ni watoto na tegemezi kwa wazazi wao lakini baadaye watakuwa watu wazima wanaopaswa kujitegemea. Matatizo mengi yanayotokea katika ndoa nyingi leo, yamechangiwa na malezi mabaya wakati wa utoto, hivyo kuathiri makuzi yao.

Wataalamu wa saikolojia wanabainisha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya yote yanayoendelea maishani mwetu leo yametokana na makuzi yetu tukiwa watoto. Kwa mantiki hiyo, watoto wanahitaji malezi bora kwa ajili ya kujenga msingi imara wa maisha yao ya baadaye.

Waswahili wanasema mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo na Neno la Mungu linasema: "Kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna," hivyo malezi bora ya watoto ni wajibu muhimu wa wazazi.

Ni jambo la kawaida kwamba watu waliolelewa katika familia tofauti wanaweza kutofautiana kuhusu namna ya kusimamia familia na kuhusu matumizi ya fedha. Wanaweza kutofautiana kuhusu fedha wanazopata kutokana na ajira au biashara. Kunapokosekana uwazi na uaminifu kuhusu fedha zao, hasa pale zinapopatikana, zinapopungua au kukosekana katika utunzaji wa familia, husababisha ugomvi na shida katika uhusiano.

Usiri katika mambo ya fedha au mali huhatarisha uhai wa ndoa. Uwazi na ukweli katika mambo ya fedha ni jambo muhimu sana. Ni jambo la msingi kwa wanandoa kuelewana juu ya mapato na matumizi ya fedha pia malengo ya kiuchumi ya muda mrefu na muda mfupi.

Uwazi na maisha yenye mshikamano ni jambo la msingi kwa wanandoa, hivyo wanandoa wanapaswa kutengeneza mazingira ya namna hiyo. Waepuke usiri juu ya fedha na mali zao. Usiri juu ya fedha na mali umekuwa chanzo cha maumivu na migogoro katika ndoa nyingi, hasa pale mke au mume anapogundua kuwa alifichwa kuhusu jambo fulani.

Mfano, imetokea mahali pengine mke au mume anaweza kununua kiwanja, gari, kujenga au kununua nyumba, kukopa fedha benki, kusaidia ndugu kifedha au kuanzisha mradi fulani bila mwenzi wake kujua bila mwenzake kujua. Kwa ujumla, kumekuwa na usiri mkubwa miongoni mwa wanandoa juu ya vipato vyao.

Limekuwa jambo la kawaida wanawake wengi kutokujua vipato vya waume zao. Hali hii imekuwa msumari wa moto au mwiba mchungu katika mioyo ya baadhi ya wanandoa, hivyo kusababisha wanandoa kutokuaminiana.

Hatua hiyo husababisha pendo la ndoa kudumaa kisha mapenzi yanakauka. Kila mmoja anapoteza hisia na mvuto kwa mwenzake. Ndoa inabaki kuwa kama boksi la zawadi lililofungwa vizuri kwa nje na kupamba wa lakini ndani yake hakuna kitu. Kumbuka kupoteza hisia ni kupoteza uhai wa ndoa.

Ni muhimu na busara wanandoa wazingatie sera ya uwazi juu ya kile wanachokipata na wanachotaka kufanya. Wafikirie athari zinazoweza kutokea kutokana na uamuzi ya kuwa wasiri na waongo kuhusu vipato vyao na matumizi ndani ya ndoa. Kama kuna hali ambayo ni kikwazo kwa mke au mume inayopelekea kutokutaka kuwa muwazi kwa mwenzake, yafaa wanandoa kujenga tabia ya kupenda mazungumzo kwa lengo la kusaidiana, kurekebisha hali iliyopo na kuleta uponyaji katika ndoa.

Kutembea na machungu moyoni huathiri afya ya akili na mwili hata kusababisha kifo. Wanandoa wanapaswa kuwa na muda wa pamoja ili kupata nafasi ya kujadiliana kwa upendo na upole, kushauriana na kushirikishana hisia zao. Mazungumzo hujenga boma zuri. Kuweka vinyongo moyoni hushawishi visasi na roho ya visasi haileti suluhu, bali huongeza maumivu na kuondoa uwepo wa Mungu.

Kutoshirikiana na kutowajibika katika ndoa, husababisha manung'uniko na mpasuko, hivyo wanandoa wanapaswa kuwa na nia moja katika kuwaza, kupanga na kutenda. Uwepo wa mipango ya pamoja iliyotanguliwa na uwazi ni chanzo cha ustawi wa kiroho, kiuchumi na kifamilia ndani ya ndoa.

Fedha au mali walizozipata kutoka kwa wazazi wao wakati wa kuagwa, harusi au ndani ya ndoa zitakuwa zao pamoja na watoto wao badala ya mwezi mmoja kuona ni zake na kwamba ndiye mwenye nguvu ya kiuchumi ndani ya ndoa. Fedha na mafanikio visiondoe utu, thamani na nafasi ya mke au mume ndani ya ndoa.

Kila jambo katika ndoa ni la wanandoa wote. Kuwe na makubaliano kuhusu mambo ya msingi ya kufanya katika maisha ya ndoa. Uwazi katika kupangilia vizuri masuala ya fedha kutawezesha kujenga ndoa imara.

Ni muhimu wanandoa kuelezana bayana juu ya vipato vyao, mali zao na jinsi watakavyovitumia kwa manufaa yao, watoto walio nao au wanaowatarajia na misaada

Ndoa imara huongeza uhai wa ndoa na maisha ya wanandoa na husababisha familia Imara. Familia imara husababisha jamii imara na jamii imara husababisha taifa imara.

Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare) inayojihusisha na masuala ya Ndoa na Malezi ya Watoto. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz"

# MAISHA

SEPTEMBA 20, 2020
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




## HARUSI

Ukurasa 12



**Wazazi wakali husaidia wabakaji**

Ukurasa 10



## MAISHA NI NYUMBA

Umuhimu wa kupangilia choo, bafu sehemu moja



**Massage ina faida nyingi mwilini**

Ukurasa 14



# Toka hivi na koti 'valvet'

Ukurasa 13

# Wazazi wakali husaidia wababakaji

INAPOTOKEA, mtaani kwenu, ukasikia kuwa mtoto fulani wa miaka minne au sita amebakwa na 'mbaba' au 'mkaka' fulani wa mtaani, linalozungumzwa na watu wengi ni kumtupia shutuma mbakaji.

Bahati mbaya zaidi ni kuwa kesi nyingi za ubakaji zinazofanyika mitaani kwetu ni zile zinazowahusu watoto waliofanyiwa vitendo hivyo kwa muda mrefu. Wamenajisiwa zaidi ya mara moja.

Utasikia ikielezwa mama wa mtoto aligundua jambo hilo wakati akimuogesha mwanae au watoto wengine wanaocheza na mtoto wake wamekwenda 'kumsemea' mwenzao kwa kufanyiwa 'mchezo mbaya'.

Na inapokuwa hivyo, mtoto kubakwa, mzazi huja juu kwa ukali na kumuliza mtoto ni nani aliyemfanyia hivyo huku fimbo ikiwa mkononi au ikiwa inamchapa mtoto huyo ili aseme ni nani aliyemfanyia hivyo.

Ukirejea simulizi zinazotolewa na watoto waliobakwa, utasikia wakisema kuwa wabakaji wao waliwatisha kwa maneno makali, kama 'ukisema tu, nakuchinja', ili kuwatia hofu ya kutowaeleza wazazi wao juu ya jambo hilo.

Kwa vitisho na hofu za namna hiyo na ule ukali unaoonyeshwa na wazazi katika visa vingi vya watoto 'kuchezewa mchezo mchafu', ndipo wabakaji wanapoweza kuendeleza vitendo hivyo kwa muda mrefu.

Cha kushangaza ni kuwa watoto hao hao, wanaoogopa vitisho hivyo vya wabakaji, ni wepesi mno kuwaeleza wazazi wao juu ya matukio mengine ya ajabu yanayotokea mtaani lakini ni wazito kuelezea 'mchezo mbaya' waliofanyiwa. Utajiuliza, ni kwa nini?



Denis Munga, mtaalamu wa saikolojia ya watoto, anasema tatizo kubwa linalowafumba midomo watoto wasiongelee juu ya matukio ya kufanyiwa 'mchezo mbaya' ni malezi ya wazazi juu ya maeneo ya ujinsia. Anasema:

"Kwa malezi ya jamii zetu, wazazi huwa hawana ujasiri wa kuzungumza na watoto juu ya sehemu za jinsia. Hakuna mzazi mwenye uthubutu wa kuzungumzia jambo hilo kabisa kwa sababu ya unyeti wa sehemu zenyewe.

"Lakini zipo njia rahisi sana za kuzungumza na mtoto juu ya sehemu hizo tena kirafiki tu na mtoto akaelewa kuwa hapaswi kuguswa sehemu hizo na mtu ye yote yule na akifanyiwa hivyo inampasa aende akamueleze mzazi.

"Hili linatakiwa lianzie mtoto anapokuwa na uwezo kujifahamu. Wakati mama anamvalisha nguo mtoto wake anaweza kumwambia kirafiki tu; 'mtu akikuchezea huku uniambie eeh' au maneno mengine mepesi atayoelewa bila ukakasi."

Munga anasema zipo njia nyingi wanazotumia kina mama kuwafundisha watoto wakike juu ya kujistiri kijinsia na wanaweza kutumia njia hizo kuongea kirafiki na watoto wao ili kuwahadharisha wanapoguswa maeneo hayo lazima aseme.

Lakini la msingi zaidi, Munga anahusia wazazi kujenga urafiki na watoto wao na kuongea nao mara kwa mara juu ya maeneo ya ujinsia pale wanapowaogesha na kuwakumbuksha juu ya kuzungumza pindi mtu mwingine anapowagusa sehemu hizo.

## NA KHAMIS KIDAGO 0657 207168

## QUIZ

1. Badili nomino zifuatazo za kifaransa kuwa vitenzi kwa kifaransa.

Mfano: Un emploi – Il emploie.

- Un travail - ………………………
- L'ennui - …………………………
- Un entretien - ……………………..
- Un envoi - …………………………
- Un essai - …………………………
- Le flair - ………………………….
- Le gel - ……………………………
- Le maintien - ……………………
- L'oubli - ………………
- Un pari - ………………..
- Un pli - ……………………
- Le rappel - …………………
- Le recours - ………………
- Le recul - …………………
- Le réveil - …………………
- Un salut - …………………..
- Un signal - ……………………
- Un souci - ……………………
- Le soutien - ……………………..
- Le tri - ………………
- Le cri - ………………
- Un trou - ………………
- Un vol - ………………..
- Le viol - ………………..
- Un zigzag - …………..

2. (Viable) au (vivable)?

¬ Le métier de professeur n'est pas ……………..financièrement.

3. (Conjoncture) au (conjecture)?

¬ Se perdre en……………

4. (Prodige) au (prodigue)?

¬ Joseph est un enfant………………

5. (Prescrire) au (proscrire)

¬ La vente de cigarettes aux mineurs est…………………par la loi.

6. (Notable) au (notoire)?

¬ Une perte……………….

7. (Comprénsif) au (compréhesible)?

¬ Mon père a été…………………….. sur le fait que je ne souhaitais pas faire le même métier que lui.

8. (Affectation) au (affection)?

¬ Ce chien est d'une……………… sans bornes pour son maître.

9. (À l'attention de) au (à l'intention de)?

¬ Une lettre………………………de Bob Rasha.

10. (Près de) au (prêt à)?


¬ Il n'est pas…………….y arriver.

11. (Allocation) au (allocution)?

¬ Son…………………n'a pas convaincu les électeurs.

## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA

MAONGEZI haya ya mke na mume yanaweza kukuvunja mbavu

**Mke:** Mimi kesho nakwenda Uingereza, nikirudi nikuletee zawadi gani?

**Mume:** Mi sijui, unaweza niletea chochote

**Mke:** We omba halafu utaona.

**Mume:** Niletee msichana wa kazi wa kizungu.


Mke aliporudi safari.

**Mume:** Zawadi yangu iko wapi?

Mke: Subiri ndani ya miezi tisa utampata msichana wa kizungu

SWALI

Mkoa gani unalima zao la korosho kwa wingi hapa Tanzania?



Alichokifanya daktari

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Sherehe aliyoandaa mkwe ilivyobomoa ndoa yangu!

MPENZI msomaji, karibu tena katika safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo, kujua yaliyojiri ndani ya familia zetu. Wiki iliyopita tulimsikia mama mmoja akijutia muda aliopoteza kwenye ndoa baada ya mume kukusudia kumpa talaka.

Wanandoa hawa wameishi kwa takriban miaka minane bila kupata mtoto. Lakini sasa mume anataka kumpa talaka mahakamani kwa sababu ambazo bado hajaziweka wazi. Hebu sikia kimbwanga kingine, ndoa iliyosambaratika muda mfupi baada ya mkwe kuwaandalia sherehe ya kuwapongeza.

Kabla sijaendelea, hebu tuelimishane mambo machache ya msingi kabisa. Katika ulimwengu wa roho, (ule ulimwengu usioonekana), yapo mambo mengi yanatokea lakini sisi wanadamu hatuyaoni kwa macho ya mwilini.

Vita vyovyote huanzia kwenye ulimwengu huo, kisha hujifunua katika ulimwengu huu tunaouona kwa macho yetu. Kwa mfano, watu wanaweza kukaa kwa siri kupanga njama ya kumuangamiza mtu fulani pasipo mtu huyo kujua. Kisha njama hizo zinakuja kutekelezwa kwa vitendo.

Isitoshe, vipo vita vya ndani ya mtu vinavyoshambulia nafsi ya mwanadamu. Vita hivi humtafuna mwanadamu taratibu, na kama hatafahamu namna ya kuvishinda anaweza kuangamia kabisa.

Vita vya ndani ya mtu ni kama vile hasira ya ghafla, huzuni, chuki, kuchanganyikiwa, kujikataa, upweke, mafarakano ya ndugu na kadhalika. Lengo la vita ya ndani ni kuhakikisha mwanadamu anakosa furaha akiwa hapa duniani.

Mpenzi msomaji, baada ya maelezo hayo kuhusu vita vya ndani, hebu sasa sikia kituko hiki kama wanavyoeleza wanandoa hawa, nikianza na mwanamke ambaye nilikutana naye kanisani.

Akasema kwamba alifunga ndoa mwaka 2011 lakini miaka miwili mama yangu akatuita kwa sherehe ya kutupongeza. Baada ya sherehe ile ukazuka mzozo kati yake na dadake, hali iliyosababisha mume kuondoa na hakurudi tena.

Nikataka pia kumsikiliza mume ambaye alimtelekeza mkewe kwa miaka saba, akafunguka na kusema hivi, "sherehe aliyoandaa mama mkwe wangu, ndiyo ilikuwa chanzo cha kutengana kwa miaka saba ila tumerudiana.

Baba huyu anasema hivi, "Mimi ni mkazi wa Arusha. Nilifunga ndoa na mke wangu huko Arusha mwaka 2011. Lakini mwaka 2013 ndoa hiyo ikasambaratika. Mke wangu ni mwenyeji wa Musoma mkoani Mara.

Miaka miwili baadaye, mama mkwe akatuita Musoma kwa ajili ya kutufanyia sherehe kwa ajili ya ndoa yetu. Kesho yake wakati tunajiandaa kufungua zawadi, mke wangu akamkumbusha dada yake fedha alizokuwa anamdai.

Dada yake akakasirika kudaiwa, ukazuka mzozo mkubwa kiasi kwamba haikuwezekana kusuluhishwa. Baada ya kuona hakuna muafaka siku nzima, mimi nikaondoka na kumuacha mke wangu wayamalize ndipo nitakapomrudia.

Tokea wakati huo, sikuwasiliana tena na mke wangu hadi mwaka huu nilipomtafuta akaniambia yupo Dar nami nikamfuata. Hivi sasa nimebahatika kupata kazi na maisha yanaendelea.

Mpenzi msomaji, tazama jinsi nguvu asi zinavyofanya kazi kati ya wanadamu. Watu wengi leo walioko kwenye ndoa wanalia sana, huku wengine wakijuta kwa uamuzi waliofanya wakati wa kuoa au kuolewa.

Wengi hawatumii muda mwingi wa kumuomba Mungu kwa habari ya wenza wao, Wengi walikurupuka tu, huku wengine wakiruhusu hisia zao kwa wakati ule eti zi-wachagulie mwenza.

Wapo waliovutiwa na muonekano wa nje bila kusikiliza sauti ya Mungu kuhusu uhusiano. Wengine walijikuta wakioa au kuolewa kwa sababu ya vitu, na sasa wanajutia.

Kilichosababisha wanandoa hawa hata wakarudiana tena, maana yake walikuwa wanapendana. Tatizo hapo ni kwamba ipo nguvu isiyoonekana ambayo ilisababisha kutengana kwao.

Yawezekana yupo mtu alikuwa hataki mwanamke huyo aolewe au mwanamume huyo aoe. Pengine wapo watu walikuwa wanawataka lakini wao wakaamua kuambatana na kufunga ndoa.

Na hicho ndicho nadhani kilitokea. Ni muhimu sana kumshirikisha Mungu katika kila jambo tulifanyalo ili tuwe na mweleko sahihi katika maisha yetu ya kila siku.

Bila shaka msomaji wangu umejifunza jambo la faida kwa wanandoa hao. Je, unayo maoni, ushauri kwa wanandoa wenye mapito ya aina hii? Je, unacho kisa unapenda tukijadili pamoja kwenye safu hii? Nitumie kupitia ujumbe mfupi kupitia 0715268581. Namba hii ipo pia Whatsap. Imeandaliwa na Flora Wingia Tukutane wiki ijayo.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Mapito ya wanyamapori yaheshimiwe vinginevyo tujiandae maafa kwa utalii

CHANGAMOTO kubwa inayokabili mapito ya wanyamapori (Shoroba) na maeneo ya mtawanyiko ni kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo ikiwamo kusajili vijiji, mashamba na makazi ya watu ambayo yameongeza migogoro baina ya binadamu na wanyama.

Mapito ya wanyamapori hufahamika kama shoroba ambazo zimetambuliwa katika Sheria Namba 5 ya Wanyamapori ya mwaka 2009 na kanuni zake, ikielezwa haitaruhusiwa kufanyika shughuli zozote za kibinadamu katika maeneo hayo.

Umuhimu wa shoroba na maeneo ya mtawanyiko ni katika kulinda ikolojia na utoa wa asili wa eneo husika, kwa kuhakikisha wanyama wanapita kutoka eneo moja lililohifadhiwa kwenda kwingine kwa ajili ya kupata mahitaji ya miili yao kama madini, kuzaliana na kubadili mazingira kulingana na majira ya mwaka, faida ambayo huipa nchi kwa watalii kuja kuwaona anyama hao kwa gharama kubwa.

Wanyama hawana mipaka ila wanajua njia zao za asili za kupita kila wakati ili kwenda eneo moja hadi lingine. Inapotokea hakuna njia ya kupita maana yake anabaki kwenye kisiwa na madhara yake ni kuzaliana kaka, dada, mama, na baba yaani mwisho kinapatikana kizazi hicho hicho ambacho kinakuwa dhaifu na huenda kikapotea.

Iko mifano ya kupotea kwa wanyama kama simba katika nchi za Ulaya na Afrika Magharibi na kwa sasa takwimu zilizotolewa na Mtafiti wa Simba wa Ikolojia ya Tarangire Manyara, Dk. Bernad Kissui, zinaonyesha idadi ya wanyama hao barani Afrika ikadiriwa kuwa ni zaidi ya 30,000 na kati yake 15,000 wanapatikana Tanzania, huku baadhi ya nchi hazina simba kabisa.

Kissui anasema kwa ikolojia ya Tarangire Manyara yenye ukubwa wa kilomita za mraba 35,000 idadi ya simba wanaouawa na wananchi kwa kuwekewa sumu kwenye mizoga, kupigwa risasi na mishale inaongezeka na hiyo inatokana na wanyama hao kupita katika mapito hayo kwenda upande mwingine.

Mathalani, shoroba ya Kwakuchinja inayounganisha hifadhi ya Tarangire na Ziwa Manyara, imevamiwa na shughuli za kibinadamu kiasi cha watu kuanzisha makazi na wanyama kama simba wanapopita hujikuta wameingia kwenye maboma na kula mifugo.

Hali inazidi kuwa ngumu kila uchao kwa kuwa watu wanaongezeka na siasa inashika hatamu kwamba kwa watu wanapokuwa katika eneo la shoroba wanahesabika ni wapigakura na kiongozi wa kisiasa hakubali waondolewe. Kila uchao kuna migogoro ya watu kuuawa, kujeruhiwa na mifugo kuliwa na wanyamapori pamoja na uharibifu wa mazao.

> "Ziko jitihada mbalimbali zinafanyika kwa kushirikiana na wadau kama USAID kufungua shoroba ambazo zilifungwa ikiwamo kujenga barabara kwa kuzingatia maeneo ya mapito ya wanyama na mtawanyiko.

Mtafiti huyo ambaye aliwaeleza waandishi waliokuwa katika ziara ya kuandika habari za utalii na uhifadhi kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), anasema wastani wa simba 20 huuawa kwa mwaka jambo ambalo ni tishio kwa ustawi wa utalii nchini.

Ziko jitihada mbalimbali zinafanyika kwa kushirikiana na wadau kama USAID kufungua shoroba ambazo zilifungwa ikiwamo kujenga barabara kwa kuzingatia maeneo ya mapito ya wanyama na mtawanyiko, kwamba barabara inapita juu na wanyama chini au barabara inapita chini na wanyama juu, kuhakikisha maeneo husika yanatumika kwa manufaa ya wanyama na binadamu.

Katika shoroba ya Kwakuchinja, kwa mfano, kuna barabara ya Arusha - Babati ambayo hupitisha magari mengi na kwa utafiti uliofanywa na mtaalamu huyo, umeonyesha kila siku zaidi ya mnyama mmoja hugongwa na gari na wachache sana wamekamatwa na kuchukuliwa hatua.

Bila utashi wa kiasiasa wa kuziangalia shoroba na maeneo ya mtawanyiko kwa jicho la pekee upo uwezekano mkubwa wa kupotea kwake na athari kubwa kwa wanyama ikiwamo kupotea kwa aina fulani ya wanyama.

Katika baadhi ya maeneo yaliyohifadhiwa kuna aina ya wanyama inapotea kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujangili na kushindwa kuzaliana na wengine badala yake kuzaliana wale wale na mwishowe kuwa na kizazi dhaifu ambacho hupotea.

Ni lazima wadau wote muhimu wa utalii wakatambua umuhimu wa mapito ya wanyama na tayari Mamlaka ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) mwaka 2009 ilitoa utafiti ulioonyesha kuwa ifikapo mwaka 2050 zitabaki shoroba mbili pakee.

Watafiti wamemaliza kazi yao ya kufanya utafiti na kuweka wazi matokeo halisi ikiwamo kuonyesha nini kitatokea baadaye, hivyo kama sekta ya utalii ni muhimu kwa maendeleo ya Tanzania, basi ni lazima ilindwe na hatua madhubuti zichukuliwe kuhakikisha wanyama wanaendelea kuwepo na shughuli za kibinadamu zinaendelea kuwepo.

***Mungi ibariki Afrika***
***Mungu ibariki Tanzania***

## HARUSI







Chereko chereko zilirindima katika msikiti wa Bakhresa, Chamazi Complex, jijini Dar es Salaam, baada ya Shamacon Pratap Singh kufunga ndoa na Rahma Ally Salum, mfanyakazi wa The Guardian Limited na kunogeshwa na sherehe iliyofanyika ukumbi wa Sabasaba.





## MITINDO



# Toka hivi na koti 'valvet'

UNAPATA furaha kama siku moja watu watasifia vazi ulilovaa, pamoja na kukupa wasifu mzuri.

Koti la aina ya 'Velvet' ni moja ya vazi linalompa mtu taswira nzuri na muonekano wa kuvutia pale anapovaa.

Ingawa vazi hili lilianza kuvaliwa zamani, lakini thamani yake bado ipo kubwa na mara nyingi inahusishwa na watu wenye maisha ya juu kama wasanii, watu maarufu na viongozi wa serikali.

Hata hivyo, watu wengine nao wameanza kuvaa kutokana na wabunifu kuendelea kutoa aina nyingi ya makoti hayo.

**UTATOKAJE?**

Velvet inapendeza kuvaa sambamba na nguo za aina na rangi mbalimbali.

Hata hivyo, kama si mtaalamu wa mavazi, unaweza kumshirikisha mtu anayefahamu suala la mitindo ili kukupa ushauri.

Kwa mfano, koti la 'Velvet' unaweza kuvaa na pensi ya denim.

Pia inapendeza zaidi ukivaa na Jeans au suruali ya kitambaa.

Haitoshi, koti la 'Velvet' linakwenda vizuri kwa kuunganishwa na sketi ya aina tofauti au unaweza kuongezea na sweta.

Kwa mfano, unaweza kuvaa koti la Velvet, ikiambatana na suruali nyeusi au kijivu na blauzi nyeupe.

**VITO HIVI VINAENDANA**

Ili kuweka mng'aro wa kipekee, unashauriwa kuvaa mapambo mengine kama shanga, pete za plastiki, mkufu na saa ya mkononi.

# UREMBO



## ‘MASSAGE’ YA ASILI

# Ina faida nyingi mwilini

MWILI ukichoka, basi kila kitu kinakwenda vibaya katika viungo vya binadamu.

Hata katika suala la urembo, kila siku mwili unatakiwa kuwa na nguvu ili uweze kuboresha afya ya viungo vyote muhimu kama ngozi, mishipa ya fahamu na mng’aro asilia.

Kuchua au ‘Massage’ ni moja ya njia ambayo ina uwezo mkubwa wa kurudisha nguvu ya mwili pamoja na kuongeza mng’aro wa ngozi.

Baadhi ya watu kila siku wanapiga hodi katika vituo vya ‘massage’, lakini kazi hiyo unaweza kufanya nyumbani kwa gharama nafuu.

Unaweza kutuma vitu vya asili kama Mafuta ya karafuu au Unga wake, binzali ya manjano, unga wa liwa, marashi ya rose na mafuta ya mzaituni kwa ajili ya kuchua mwili.

**JINSI YA KUFANYA**

Unatakiwa kuoga vizuri kabla ya kuanza kuchua mwili, inaweza kufanywa kitandani, kwenye mkeka au chini.

Anza kusugua mwili kwa kutumia unga wa liwa na unga wa karafuu uliochanganywa na marashi ya rose.

Sugua mwili mpaka uhisi uchafu na nongo zote zimeisha. Baada ya hapo oga tena na kisha upake mafuta ya mzaituni, nazi, karafuu au ya ufuta. Tutumia nguvu kiasi sehemu ya kiunoni.Utaendelea kuchua hadi utakaporidhika kuwa mwili upo sawasawa.

**FAIDA ZAKE**

Pamoja na kuboresha mwili, kuchua inasaidia kuondoa uchafu mwilini na kupunguza maumivu makali, inakupa pumziko na kuondoa msongo wa mawazo.

Massage husaidia kuondoa kovu la jeraha, huzuia kansa ya ngozi na matiti na huboresha mmeng'enyo wa chakula.

# MAPISHI

## Na Mary Geofrey

## Namna ya kutengeneza ‘coleslaw’





COLESLAW ni aina ya saladi ambayo hutumika kwa ajili ya kula na vyakula mbalimbali.

Kwa mazingira ya Kitanzania, Coleslaw tumezoea kuona ikitumika zaidi katika shughuli mbalimbali na kwenye hoteli za kifahari.

Leo tutaelekezana namna ya kutengeneza ili kila familia iwe na uwezo wa kuandaa saladi hii badala ya kusubiri kuila kwenye shughuli.

**Mahitaji**

Kabichi iliyokatwa nyembamba vikombe viwili na karoti moja iliyokwaguliwa.

Kadhalika kitunguu kilichokatwa vipande vyembamba, mtindi (yoghurt) au mayonnaise nusu kikombe, limau robo na chumvi kiasi.

**Matayarisho**

Changanya vitu vyote mpaka mchanganyiko wako uwe vizuri katika bakuli moja safi.

Baada ya hapo iweke kwenye friji kwa muda mchache ili chumvi na limao viingie katika kabichi na carrot.

Ukishafanya hivyo, Caleslaw yako itakuwa tayari kwa kuliwa na hii ni aina mojawapo ya saladi na mara nyingi pindi watengenezapo hupenda kutumia mayonnaise.

Unaweza kutumia mayonnise au yogurt na unaweza kulia na chips, nyama au chochote upendacho.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Umuhimu wa kupangilia choo, bafu sehemu moja



BAFU na choo ni vitu muhimu sana katika nyumba hususani vinapojengwa kwa ubora unaostahili.

Katika nyumba nyingi zinazojengwa sasa, ujenzi wa choo na bafu vimekuwa vikiwekwa katika sehemu au chumba kimoja na kujengewa kila kimoja na mfumo wake wa kupitisha maji, bila ya kuathiri nyingine.

Rosemary Kwinuka, ni mtaalamu katika eneo hilo, anayesema sehemu linapokuwapo bafu kunatakiwa vitu muhimu vitatu. Hapa anataja sinki la kunawa mikono, mahali pa kupiga mswaki na choo.

"Tunapozungumzia bafu bora ni lile ambalo lina 'full component,' yaani lina sehemu zote za kuogea, kupiga mswaki na choo. Cha muhimu ni kuangalia fundi anapangilia vipi sehemu ya kupita maji ya sehemu zote hizo bila kuleta athari," anasema Kwinuka.

"Ukitengeneza kila sehemu peke yake, yaani sehemu ya kuogea, sinki, choo na ya kupigia mswaki peke yake utaishia kutoboa kila mahali na utaharibu zaidi ukuta wako. Kuna namna ya kutengeneza kitaalam vitu vyote hivyo vikatumia ukuta mmoja au mbili bila kuleta atahari."



Anafafanua kwamba, mara nyingi choo kinapaswa kuwekwa katika sehemu ambayo ni ya mwisho na inakuwa rahisi kupitisha mfumo wa utoaji uchafu, bila kuathiri sehemu nyingine.

"Pia mpangilio wa vitu hivi vyote katika ukuta mmoja, ni bora zaidi kwa sababu mbali na kuzuia kuharibu ukuta, lakini inasadia kupunguza gharama na mabomba."

MPANGILIO

# Dondoo muhimu usafi asilia chooni

CHOO kina umhimu katika nyumba, lakini suala la usafi ni jambo la kipekee zaidi ili kukamilisha makazi yako.

Hizi ni baadhi ya njia asilia unazoweza kuchukua ili kukifanya choo kiwe kisafi na kinachovutia.

**Dirisha**

Kama dilisha la choo ni la kioo, unaweza kusafisha kwa mchanganyiko wa maji na vinegar. Pia futa kwa kutumia kitambaa au karatasi.

**Mabomba ya kuogea**

Kama unatumia mabomba ,unaweza tumia kitambaa kufutia.

**Sakafu**

Safisha sakafu ya marumaru kwa vinegar na maji, pia utafanya hivyo kwa kibebea sabuni, makabati na sehemu ya kuhifadhia taulo.

Kwa maru maru za ukutani na milango kwa dawa hizo husafisha kwa ufanisi mkubwa.

**Jakuzi**

Baking soda na maji utasafisha kwa bomba la mvua na jakuzi, kwa sehemu yenye uchafu mwingi tumia vinegar pekee.



**vyoo**

Mwagia baking soda ndani ya choo na kisha igande, weka kimoja cha vinegar nyeupe ndani ya choo.Tumia brashi nzuri ya kusugulia choo utaona madoa yanatoweka.

**Manukato**

Ili kuondoa harufu mbaya, unaweka jivu au maua ya waridi kuweka harufu nzuri.

# KATUNIKA KI'DOMOKRASIA

**BY ABDUL KINGO - 2020**

**SMS - 0621 412 879**

**JUKWAANI**
















***KINYUNYIZO CHA LEO...**

***...HAKUNA POSHO NDOGO...***

## HABRI KIMATAIFA

# Kifo cha jaji chazua tafrani Marekani

**WASHINGTON, MAREKANI**

JAJI wa Mahakama ya Juu ya Marekani, Ruth Bader Ginsburg, ambaye alikuwa mwanamake wa pili kushika nafasi hiyo, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 87.

Kifo chake kimetokea wiki sita, kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu wa Rais wa nchi hiyo.

Baada tangazo hilo, huenda ikaibuka mapambano makali ya kisiasa kama Rais Donald Trump, atamteua mtu mwingine.

Msuguano utakuwa kati ya Bunge la Wawakili ambalo lipo chini ya Democratic na Seneti linalodhibitiwa na Warepublican kwa ajili ya kuidhinisha uteuzi mpya.

Ginsburg alikuwa na siasa za kiliberali aliyetambulika kwa kutetea haki za wanawake na jamii za walio wachache.

Kiongozi wa Maseneta Mitch McConnell, alisema Seneti itapiga kura ya kuidhinisha au kupinga jaji atakayependekezwa na Trump, hata kama kuna uchaguzi.

Rais Trump alimuita Ginsburg kama mwanamke wa ajabu na hakusema chochote kuhusu mtu atakayechukua nafasi yake.

*DW*



Raia wa Marekani, Felipe Morales, akiangalia gari lake baada ya kusombwa na maji yaliyotokana na kimbunga Imelda kilichoipiga jiji la Houston juzi. (**PICHA: AP**)

# Rais wa Peru anusurika kung'olewa

**LIMA, PERU**

RAIS wa Peru, Martin Vizcarra, amenusurika kuondolewa madarakani kupitia mchakato wa kura za kutokuwa na imani naye.

Upigaji wa kura hiyo ulifanyika siku ya Ijumaa, wabunge kutoka upande wa upinzani walishindwa kupata wingi wa kura zilizohitajika kumuondowa madarakani kiongozi huyo.

Bunge la nchi hiyo lilipiga kura wiki iliyopita kuanzisha mchakato wa kumuondowa madarakani kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 57, kwa tuhuma ya kukosa maadili.

Ilidaiwa Rais Vizcarra aliwashinikiza wasaidizi wake kutoa taarifa za uwongo wakati wa uchunguzi wa rushwa.

Kiongozi huyo alimlaumu spika wa bunge, Manuel Marino, kuwa ana njama za kumuondoa madarakani na kujaribu kupata uungaji mkono wa jeshi.

*DW.*

# Ulaya kuwekea vikwazo kampuni tatu

**PARIS, UFARANSA**

UMOJA wa Ulaya unajiandaa kutangaza vikwazo dhidi ya kampuni tatu kutoka Uturuki, Jordan na Kazakhstan.

Hatua hiyo inachukuliwa kama adhabu baada ya kampuni hizo kutuhumiwa kukiuka vikwazo vya silaha nchini Libya.

Taarifa hiyo ilitolewa na mwanadiplomasia ambae aliliambia shirika la habari la Ufaransa la (AFP) kwa sharti la kutotajwa jina lake.

Umoja huo umeweka mpango maalum wa kuweka ulinzi wa bahari katika eneo la Pwani ya Libya.

Nchi ya Uturuki ni moja ya wafadhili wakubwa wa serikali inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa, ambayo ipo katika vita kamili kwa mbabe Khalifa Haftar.

*DW*

# China yalaani kuzuiwa mitandao yake

BEIJING, China

CHINA imelaani hatua ya Marekani, kupiga marufuku matumizi ya programu za simu za mitandao ya kijamii za TikTok na WeChat.

Marufuku hiyo inaanza kutekelezwa leo, baada ya Rais Donald Trum, kuweka saini amri ya kuzia mitandao hiyo kutoka China, kufanya kazi ndani ya taifa hilo.

Akijibu swali la mwandishi wa habari, msemaji wa Wizara ya Biashara, alisema hatua hiyo inaathiri haki za kisheria za kampuni husika, kwa kuvuruga utaratibu wa kawaida wa soko.

Hata hivyo, alisema serikali yao itajibu suala hilo kwa kuchukua hatua muhimu kwa lengo la kuyalinda maslahi ya Wachina.

Rais Trump, mara kadhaa alikuwa akitishia mitandao hiyo akieleza ni kwa ajili ya kulinda usalama wa taifa na wasiwasi wa udukuzi wa taarifa za watu.

**DW**

# Ndege ya mizigo yaanguka Somalia

Mogadishu, SOMALIA

NDEGE moja ya mizigo imeanguka katika eneo la uwanja wa ndege wa kimataifa wa mjini Mogadishu, nchini Somalia.

Hata hivyo, haujatolewa uthibitisho wa tukio hilo na athari yake, ingawa picha zilizosambazwa zilionyesha eneo la mbele la ndege hiyo likiwa limegonga ukingo hatua chache kutoka baharini. Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Somalia imethibitisha kutokea kwa ajali hiyo katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Aden Adde.

Alama zilizomo katika ndege hiyo, zinaonyesha ni ya kampuni ya Kenya ya Silverstone.

Hata hivyo msemaji wa mpango wa ulinzi wa amani wa Umoja wa Mataifa wa Somalia, ambae alionekana katika picha za ajali hiyo, hakuweza kupatikana.

**DW**

MAKALA

# Bado kunauchanga utekelezaji demokrasia



Na Magabilo Masambu

SEPTEMBA 15, kila mwaka, dunia huadhimisha Siku ya Demokorasia ambayo ilipangwa na Umoja wa Mataifa. Siku hii ni kuikumbusha dunia kuzingatia haki za kimsingi za kidemokrasia ambazo ni pamoja na haki za binadamu kwa maana ya utawala wa sheria, haki za kijamii, usawa katika jamii kwa makundi yote, haki za kuchagua na kuchaguliwa, uhuru wa maoni ya watu na haki nyinginezo.

Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi iliyoridhia misingi ya kidemokrasia kama ambavyo imeainishwa katika ibara 8(1) ya Katiba yetu kwamba "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya kidemokrasia na haki ya kijamii na kwahiyo;(a) wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.

Bahati nzuri mwaka huu wa 2020 wakati tukiadhimisha siku ya demokrasia duniani, Tanzania ipo kwenye mchakato wa kutimiza takwa mojawapo la kidemokrasia ambalo ni kuwafanya wananchi wajipatie viongozi wake kupitia sanduku la kura ili kumpata rais, wawakilishi (wabunge) pamoja na madiwani.

Pamoja na changamoto ambazo zinajitokeza angalau takwa hili linaonekana kuwapo ndiyo maana wagombea wana uhuru wa kufanya kampeni ili kuuza sera zao kwa wananchi na waweze kuchaguliwa.

Ni ukweli uliowazi kwamba, katika ukanda huu wa bara la Afrika kutokana na uchanga wa nchi zetu hizi katika kujitawala pamoja na tamaduni tulizonazo kama waafrika, bado jambo la kidemokrasia halijapata kueleweka sawasawa kutoka ngazi za kifamilia mpaka kwa viongozi wa kitaifa.

Bado kuna kusukumana hapa na pale, kushutumiana, kulaumiana tuonapo haya basi tufahamu bado tunauchanga katika kutekeleza demokrasia ya kweli ni imani yangu kwamba safari hii itachukuwa kitambo kidogo mpaka pale itakapoeleweka tangu ngazi ya familia zetu ambazo kwa utamaduni wetu mkubwa huwa siku zote yuko sahihi.

Mara nyingi demokrasia imeonekana kuwahusu wanasiasa tu, lakini vipi kuhusu famila zetu? Je, watoto ndani ya familia wana uhuru kiasi gani wa kuchagua mambo wanayoyataka? Je sisi kama wazazi katika kuyakataa au kuyakubali mambo hayo huwa tunatumia njia gani? Ni kweli kwamba kama familia hatuwezi kukubali kila anachokitaka mtoto, lakini lazima tuwe na njia sahihi ya kuwaeleza ili wakubaliane na hali halisi za familia zetu, kwasababu pengine wakati mwingine watoto wetu wanaweza kuhitaji mambo ambayo yapo juu ya uwezo wetu au mambo ambayo yanaweza kuwa ni hatari kwao na kwasababu hawajapevuka kifikra ikawa ngumu kwao kufahamu athari za mambo hayo.

Jukumu letu kama wazazi ni kuwaeleza vizuri katika majadiliano ili waelewe na nina uhakika kama tunatumia njia sahihi za kueleza kwanini tutekeleze au vinginevyo basi ni rahisi wao kutuelewa na kutekeleza tunayoyahitaji kwaajili ya manufaa yao.

Haya yakanikumbusha maneno ya Mwl. JK.Nyerere katika kitabu chake cha Tujisahihishe (1962), uk 3. Anasema "Ni kweli kwamba demokrasia haiwezi kudumu ikiwa wachache hawatakubali matakwa ya kweli. Lakini matakwa ya wengi hujulikana katika majadiliano au mazunguzo ya waziwazi. Kadhalika matakwa ya wachache hujulikana katika majadiliano na mazungumzo. Bila wale wachache kusema waziwazi matakwa yao, majadiliano hayana maana. Wakati mwingine hata baada ya majadiliano wachache japo wamekubali kutii uamuzi wa wengi wanaweza kuendelea kuamini kwamba mawazo yao ni sawa na yaliyo ya wengi yamepotoka. Demokrasia inawapa haki na ukweli unawapa wajibu wa kuendeleza mawazo yao mpaka wengi waone kuwa ni ya kweli. Bila hivyo maendeleo katika mawazo hayawezekani"

Demokrasia ni kiini cha maendeleo kama alivyosema Mwl. JK Nyerere miaka kumi baada ya Azimio la Arusha kwa maana ya kwamba, maendeleo hutokana na msuguano wa kimawazo katika fikra za watu na walioko katika madaraka wanapata fursa ya kuwafahamu watu wanaowaongoza kupitia uhuru wa kujieleza na kufahamu vyema upungufu wao kutokana na mawazo mbadala ya wale wanaoongozwa.

Wakati tukiendelea na mchakato wa uchaguzi mkuu ambao utafanyika Oktoba 28, 2020, nimepata nafasi ya kufanya mazungumzo na baadhi ya viongozi wa vyama visivyo na uwakilishi bungeni. Shauku yangu kubwa nikitaka kufahamu kwanini inaonekana wananchi ni wagumu kujitokeza katika kampeni za vyama hivi ambavyo wengine wanaviita vyama vidogo! Kimsingi si vyama vidogo kwasababu haki za kikatiba, sheria za vyama vya siasa na sheria za uchaguzi huvitambua kama vyama sawasawa kabisa na vile vinavyojiita vyama vikubwa.

Zuberi Mwinyi mgombea wa jimbo la Arusha mjini kupitia chama cha ADA TADEA ambaye pia ni katibu wa vyama kumi na moja (11) vilivyoamua kushirikiana bila kuungana ambavyo ni TLP, ADA TADEA, SAU, AAFP, UPD, UMD, UDP, ADC, DP, CCK, na Demokrasia MAKINI. Yeye anasema sababu kubwa ni katika muktadha uleule wa wananchi wa Tanzania kutothamini maoni ya wachache, lakini si kweli kwamba vyama visivyo na uwakilishi havina sera.

***Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika.***

***Kwa maoni na ushauri***
***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Joka la Kibisa' la enzi hizooo



Na Adam Fungamwango

VIJANA wa kisasa wana msemo mmoja ambao sidhani kama wengi wanajua chanzo chake kilitokana na nini. Utasikia mtu akimwambia mwenzake "Hana lolote huyo Joka la Kibisa tu."

Wengi wanajua maana yake kuwa ni mtu ambaye anajifanya ana nguvu na anatishia kutokana na mwonekano wake, lakini ukweli ni kwamba sivyo alivyo.

Kama anajifanya ana nguvu, basi si kweli na mengine yanayofanana na hayo. Neno la 'Joka la Kibisa' lilitokana na majoka yaliyokuwa wakifugwa na kikundi maarufu cha sanaa za maonyesho wakati huo cha DDC Kibisa.

Hicho ni moja ya vikundi vya burudani vilivyokuwa vikimilikiwa na Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam (DDC). Kikundi kingine kilichokuwa kikimilikiwa na shirikia hilo ni bendi ya muziki wa dansi ya DDC Mlimani Park Orchestra yenye mtindo maarufu wa Sikinde Ngoma ya Ukae. Kwa sasa bendi hiyo inaitwa Mlimani Park Orchestra.

Nyoka hao walikuwa wakifugwa na kupewa chakula, wakiondolewa baadhi ya vitu ambavyo vinaonekana vingekuwa hatari kwa binadamu, hivyo wanabaki kama walivyo. Kwa maana hiyo wanabaki kuwa nyoka kwa umbile na kila kitu, lakini hawana hatari yoyote kwa bindamu.

Hiyo ndiyo maana halisi ya 'Joka la Kibisa'. Ina maana hana hatari wala maajabu yoyote.

Nyoka wa Kibisa walikuwa wakitumika kwenye maonyesho ya kundi hilo miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000, vikundi vya sanaa za maonyesho vilipoanza kupoteza umaarufu.

DDC Kibisa Ngoma Troup, ilikuwa inaviongoza vikundi vingi vya sanaa ambavyo vilijipatia umaarufu mkubwa miaka hiyo nchini ambavyo vilikuwa vikifanya ziara katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kufanya maonyesho, kuhamasisha utamaduni wa Mtanzania na Mwafrika kwa ujumla.

Mbali na Kibisa, kulikuwa na vikundi vingi vilivyojipatia mashabiki wengi na umaarufu kama Muungano Culture, Makutano Dancing Troupe, Ujamaa Ngoma Troupe, Mandela Theatre, Bima Modern Taarab, Super Fanaka, Reli Kiboko Yao, JWTZ, na Urafiki.

Hii ni kabla ya kundi la TOT halijaundwa mwanzoni mwa miaka ya 1990 likiwa limesheheni wasanii wengi kutoka kundi la sanaa la Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) akiwamo Kapteni John Komba ambaye alikuwa akiliongoza kundi hilo na baadaye kuongoza TOT.

Makundi haya yote yalikuwa na idara mbalimbali kama vile ngoma za asili, vichekesho, maigizo, sarakasi na kwaya, huku vingine vikiwa na taarab pamoja na muziki wa dansi.

Vikundi hivi vilikuwa na uwezo wa kupiga ngoma za makabila mbalimbali nchini Tanzania, hivyo kuwakumbusha watu hasa wale walikuwa wakiishi miji mikuu, hususan Dar es Salaam na hawajarudi kwao muda mrefu, lakini iliwafanya watoto na vijana wengi kujua utamaduni wa asili yao na hata ngoma.

Huu ulikuwa mtoko hasa wa kila wiki kwa familia nyingi. Kutokana na kutokuwapo wakati huo kwa teknolojia kama ya televisheni nchini, wazazi walikuwa wakiwachukua watoto wao wikiendi na kwenda nao kwenye vikundi hivyo.

Ndiyo maana watoto wengi wakati huo, wa rika mbalimbali, kuanzia mwaka mmoja hadi 17, walikuwa wakifurika kwenye maonyesho ya sanaa ya vikundi hivyo ambavyo vyote vilipachikwa jina moja tu la 'Kibisa.'

Haijajulikana ni kwa nini vikundi vyote hivyo vilijulikana kwa jina moja tu la 'Kibisa' lakini inawezekana kundi hilo likawa ndilo mwanzilishi wa sanaa hizo za maonyesho. Ndilo lililoonekana kuwa na wasanii wengi wakubwa na mashuhuri kama kina Mzee Majuto, Blaco, Mwanchia, Mzee Small, Makwaya Kasidi maarufu kama Saba Unusu, Alhaji Kashata na Vumbi.

Hivi vikundi ndivyo vilivyowatoa baadhi ya wasanii wa mwanzo kabisa wa maigizo ya kwenye televisheni, lakini pia hata kina Bi. Chau walitokea kwenye vikundi hivi vya sanaa.

Ni vikundi vilivyowafanya watoto wengi wa wakati huo kupenda michezo mingi tofauti kama kupiga ngoma, kucheza ngoma za makabila mbalimbali na kujifunza sarakasi. Kwa sasa ni aghalabu kuona watoto na vijana wa sasa wakifanya hivyo.

Vikundi hivi ndivyo vilikuwa kimbilio kubwa kwa burudani ya watoto kwa siku za mwisho wa juma kwa sababu isingewezekana wao kwenda kwenye muziki wa dansi.

Ingawa mara nyingi kumbi zinakuwa zile zile zinazopigwa muziki wa dansi, vikundi hivyo vilikuwa vinaanza saa 8:00 nane mchana hadi saa mbili usiku kwa Jumamosi na Jumapili na baada ya hapo unaanza muziki wa dansi mpaka majogoo.

Kwa hiyo burudani ziligawanyika kwa watoto kwenda Kibisa na mama zao, dada zao au walezi wao, huku baba yeye akienda dansi. Wakati mwingine hata kina baba, wake zao na familia nao walikuwa wanaungana kwenda Kibisa.

Vikundi vyote hivi vilikuwa vikijaza watazamaji kila vilipokuwa vikifanya maonyesho yao jijini Dar es Salaam na hata kwenye mikoa mbalimbali nchini Tanzania. Wakati wakitazama maonyesho, watoto na vijana na walezi wao walikuwa wakiburudika na vinywaji baridi na vitafunio vilivyokuwa vikiuzwa ndani ya kumbi.

Tatizo lilikuwa moja tu. Pale ngoma ya Kisukuma ambayo inaambatana na nyoka. Hapo sasa wale watoto wenye roho ndogo na mama zao utaona wanaanza kuondoka. wanaobaki inakuwa ni tafrani pale, nyoka wanapoanza kutolewa kwenye sanduku na kuwekwa kwenye sakafu la jukwaa huku wakitambaa huku na huko.

Wapo waliokuwa na ujasiri wa kupanda jukwaani kwenda kupiga nao picha. Lakini walikuwa wachache sana.

Vikundi hivi vilianza kusambaratika katikati ya miaka ya 1990. Sababu ni nyingi, lakini kubwa ni kuanza kubinafsishwa kwa mashirika ya umma, ambayo mengi yalikuwa yakimiliki vikundi hivyo.


# HADITHI

HAKUNA adui wa kudumu katika maisha na adui yako mkubwa aweza kuwa rafiki. Tatu na Zubeda walikuwa paka na panya kwa sababu ya mama mkwe wa Tatu, Bi. Mwapewa. Lakini kuna jambo limewafanya wawili hao kuwa marafiki wakubwa. Jambo hilo ni nini? Fuatilia kisa hiki cha kusisimua kupata undani kamili...

# Mama Mkwe- 3

**Na Adam Fungamwango**

(0716 350534)




ILIKUWA siku ya tatu baada ya tukio lile. Alichukua ndoo yake na kujifanya anakwenda bombani. Hiyo ilikuwa baada ya kumwona Zubeda anakwenda. Awali hakutaka kufika huko.

Alichofanya ni kumsubiri njiani ili wapishane kama vile mmoja anarudi na mwigine anakwenda. Kwa mbali alimwona Zubeda amebeba ndoo yake anarejea. Na yeye akaanza kujifanya anaongeza mwendo.

Walipokaribiana, Zubeda alianza kukunja sura. Ni kwa sababu alimwona mbaya wake. Tatu yeye alitabasamu. Zubeda alishangaa kwa sababu kila anapokutana ananuna na kuwa mwoga.

"Zubeda dada yangu, nataka nikwambie kitu. Hicho kitu ni cha manufaa kwangu na kwako pia." Alisema Tatu na kumshangaza Zubeda.

Hakujua ni kitu gani. Akabaki amepigwa na butwaa. Akawa mpole ghafla akitaka kujua hicho kitu. Akahadithiwa kila kitu juu ya mumewe Jaffar.

"Mimi nimeolewa. Halafu pia pamoja na ugomvi wetu, wewe ni mwanamke mwenzangu, siwezi kukufanyia kitu kibaya, eti nilipize kisasi hapata." Tatu alimpasha.

Awali Zubeda hakuamini. Alidhani ni njama tu za Tatu kutaka kupoza ugomvi wao, lakini kila hatua moja kwenda mbele alianza kuamini. Akaonyeshwa pia meseji za mapenzi ambazo mumewe alimwandikia Tatu.

"Nataka tulikomeshe jambo hili." Tatu alimwambia Zubeda ambaye kwake jambo lile lilikuwa kama ndoto. Hakudhani kama mumewe angeweza kutaka kumsaliti. Pia hakudhani mtu ambaye anamsakama mara kwa mara, leo amemfuata kwa heshima zote kuelezea jambo hilo zito kwake, huku akitaka walikomeshe.

"Shoga yangu hapa mimi nimechoka. Hata nguvu sina. Yaani presha inataka kunipanda hapa. Hebu nisaidie kutua hii ndoo, nikae chini, naweza kuanguka bure." Zubeda alikuwa mpole kama kidonge cha kutuliza mafua.

"Mimi sina la kusema nakuachia wewe. Tufanye nini? Tunamkomeshaje?"

"Niachie mimi."

"Shoga naomba radhi kwa yote niliyokufanyia. Sikutegemea kama unaweza kuwa na roho nzuri kama hii." Zubeda aliomba msamaha.

"Wala usijali, mimi nilijua tu mama mkwe wangu ndiye anakupelekapeleka, achana naye, yule nitamaliza naye, ila wewe tumalize suala hili. Na hapa tuondoke kabla watu hawajatuona, maana watashangaa sana. Nataka waendelee kujua kuwa sisi bado tunagombana." Tatu alimwambia Zubeda na kuagana.

**"Hapana Zubeda, hili jambo liishie hapa hapa. Asijue mtu yoyote kijijini. Tulimalize, msamehe mumeo. Mimi kuanzia leo nitakuwa shoga yako mkubwa na nitakusaidia jinsi gani ya kurudisha upendo kwa mumeo, kama mimi ninavyompenda Rashid. Nadhani ni tabia yako tu ya kutotulia nyumbani ndiyo iliyomfanya mumeo kufanya hivi," alisema na kumshangaza hata Jaffar.**

**********************

Ilikuwa saa tatu usiku. Tatu tayari alikuwa amejipamba, akapambika. Alijiandaa kwenda kukutana na Jaffar kama walivyoahidiana kwenye meseji. Mumewe hakuwapo nyumbani.

Aliondoka taratibu kwenda sehemu ambayo waliahidiana. Alimkuta Jaffar akimsubiri kwa hamu. Alifurahi kumuona. Karibu na hapo kulikuwa na nyumba ya wageni ambayo ndiyo walitaka kwenda.

"Umekuja mtoto mzuri." Jaffar alionekana kufurahi. Aliona kabisa ingekuwa siku nzuri sana kuburudika na Tatu baada ya kuchoshwa na mambo ya mkewe.

Tatu alionekana kumzungushazungusha. Dakika kumi tu baadaye, ghafla Zubeda alijitokeza.

"Kumbe ndiyo tabia yako, mwanaume hizaya we." Ilikuwa ni sauti ambayo aliizoea kusikia akiwa nyumbani. Ilikuwa ya mkewe.

Alichoshangaa Jaffar ni kwamba mfumaniwa mwenzake Tatu hakuonekana kuwa wasiwasi, lakini pia mkewe Zubeda hakumshambulia Tatu ambaye anajua kabisa kuwa hawalewani.

Wote wawili, Zubeda na Tatu walimkamata Jaffar na akashindwa kufurukuta.

"Basi jamani naombeni samahani." Alisikika Jaffar akisema huku akiwa amebanwa asijue la kufanya.

"Iwe mwanzo na mwisho kutaka wake za watu, oooh unanipenda, oooh una'ntaka. Unan'taka hiyo kwio?" Tatu alimsimanga.

"Twende nyumbani leo utakoma." Zubeda alimwambia mumewe.

"Hapana Zubeda, hili jambo liishie hapa hapa. Asijue mtu yoyote kijijini. Tulimalize, msamehe mumeo. Mimi kuanzia leo nitakuwa shoga yako mkubwa na nitakusaidia jinsi gani ya kurudisha upendo kwa mumeo, kama mimi ninavyompenda Rashid. Nadhani ni tabia yako tu ya kutotulia nyumbani ndiyo iliyomfanya mumeo kufanya hivi," alisema na kumshangaza hata Jaffar.

"Nashukuru shoga yangu, nimekusikia. Kuanzia kesho, watu watashangaa kuona niko na wewe na kila kitu nitakibadilisha katika maisha yangu. Najuta kukufanyia mambo yasiyostahili."

"Usijute Zubeda, hiyo ni mipango ya Mungu." Alisema Tatu huku akimpa moyo huyo shoga yake ambaye awali alikuwa adui yake.

Zubeda alianza kuangua kilio na kumkumbatia Tatu. Tatu naye akaanza kutokwa machozi.

Jaffar alipata kazi ya kuwabembeleza, kuwatuliza na kurudi nao nyumbani.

# DIAMOND AMPONZA ALICIA KEYS

## Kiswahili chatawala kwenye mtandao wake



BAADA ya siku moja kutambulisha albamu yake mpya, mwanamuziki wa Marekani, Alicia Augello Cook, maarufu kama Alicia Keys, mtandao wake wa instagram umevamiwa na Watanzania kiasi ambacho hata mwenyewe ameshangazwa.

Katika albamu yake hiyo aliyoita ALICIA, ambayo ameiachia jana, miongoni mwa wanamuziki walioshirikishwa, jina la Mtanzania, Diamond Platnumz limejitokeza.

Katika orodha ya nyimbo 15 ambazo zimo ndani ya Album yake hiyo, wimbo namba nne unaoitwa Wasted Energy, ndio Diamond Platnumz, ameshiriki kuimba.


Kufuatia tangazo hilo, akaunti ya mtandao wa Instagram ya Alicia Keys, tangu jana imeelemewa kwa idadi kubwa ya Watanzania, huku lugha ya Kiswahili ikiwa imetawala.

Kutokana na watu wengi kujitokeza kuwaunga mkono, wimbo wa 'Wasted Energy' unaongoza kwa kuwa na watazamaji wengi kuliko nyimbo nyingine alizowashirikisha wasanii wengine.

Kwa Alicia hii itakuwa ni Albam yake ya kwanza ndani ya miaka mitatu , tangu alivyoachia "Dirty Dancing 2" Mwaka 2017.



## Dogo Janja kumbe bangi ilimdatisha



MWANAMUZIKI wa HipHop, Dogo Janja, amesimulia jinsi bangi ilivyomchanganya akili wakati alipojaribu kuvuta.

Dogo Janja amesema siku alipojaribu kutumia dawa hiyo ya kulevya, ilimfanya awe mtu kuchekacheka ovyo.

"Mimi sivuti bangi, ningetaka kuvuta ningefanya tangu zamani kwa sababu nilikulia mazingira ya hivyo na niliona madhara yake, nilijaribu mara moja nikawa nacheka tu nikaona hainikubali" Dogo Janja amesema katika kipindi cha Salama na kinachorushwa na EATV.

## Ditto haelewi kitu urafiki wa mashaka

MSANII wa muziki wa BongoFleva,Lameck Ditto, amepinga dhana ya urafiki wa watu wa jinsia mbili tofauti, akidai jambo hilo haliwezekani kutokana na kila mmoja kuwa na hisia.

Akitoa maoni yake kwenye kipindi cha MamaMia ya East Africa Radio, Ditto amesema kuwa yeye kama mwanaume anaelewa nini kitakachofuata katika urafiki wa aina hiyo.

"Ndani ya urafiki wa mwanamume na mwanamke lazima kuna jambo limejificha, sijawahi kuona na kama wapo marafiki basi ni mmoja tu duniani, tusidanganyane mimi ni mwanamume naelewa wanaume hatuwezi labda wanawake wanaweza vumilia ila sisi hatuwezi," amesema Ditto.



## HABARI MICHEZO




# ARTETA: NILIHOFIA HATIMA YA AUBAMEYANG ARSENAL

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amebainisha hakuwa na uhakika kama nahodha wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang angeweza kukubali kubakia klabuni hapo.

Aubameyang, ambaye alifunga kwenye mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa Ligi Kuu England kwenye ushindi dhidi ya Fulham, alisaini miaka mitatu kubakia kwenye dimba la Emirates wiki hii.

Lakini kocha wa Arsenal, Arteta, amesema hakuwa kabisa na uhakika kama straika huyo raia wa Gabon atabakia kikosini hapo.

"Mara ya kwanza wakati nilipojiunga sikuwa na uhakika kabisa," amesema Arteta, ambaye aliteuliwa kuinoa timu hiyo Desemba, mwaka jana.

"Kiukweli hatukuwa vizuri kifedha na ndio nikaona uwezekano wa Auba kubaki ni mdogo sana.

"Lakini hatimaye mambo yakaenda sawa na sasa amebaki na atakuwa na sisi kwa miaka mingine mitatu."

Aubameyang alijiunga na Arsenal kutoka Borussia Dortmund Januari, mwaka 2018 na tangu hapo amefunga mabao 55 kwenye Ligi Kuu.

## Neymar, Silva, Coutinho kuiongoza Brazil

**RIO DE JAINERO,** Brazil

NEYMAR na Thiago Silva wameitwa kwenye kikosi cha Brazil kilichochaguliwa na Kocha, Tite ili kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Bolivia na Peru.

Tite ameita wachezaji 23 wakiwamo saba wanaocheza Ligi Kuu England, huku mkongwe Silva aliyesajiliwa Chelsea akitokea kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain akijumuishwa.

Nyota wa PSG, Neymar ni miongoni mwa wachezaji walioitwa pamoja na Roberto Firmino wa Liverpool, straika wa Manchester City, Gabriel Jesus, Richarlison wa Everton na Rodrygo wa Real Madrid.

Winga wa Barcelona, Philippe Coutinho, ambaye majaliwa yake hayajulikani kule Camp Nou baada ya ujio wa kocha mpya, Ronald Koeman aliyechukua nafasi ya Quique Setien pia ameitwa.

Brazil itavaana na Bolivia mjini Sao Paulo Oktoba 9, mwaka huu kabla ya kusafiri kwenda kuivaa Peru mjini Lima siku nne baadaye, katika mbio za kuwania kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka 2022.

Mlinzi wa Palmeiras, Gabriel Menino na kiungo wa Lyon, Bruno Guimaraes watakuwa kwenye kikosi hicho kwa mara ya kwanza.

Kikosi cha Brazil: Alisson (Liverpool), Santos (Athletico-PR), Weverton (Palmeiras); Rodrigo Caio (Flamengo), Danilo (Juventus), Felipe (Atletico Madrid), Renan Lodi (Atletico Madrid), Marquinhos (Paris Saint-Germain), Gabriel Menino (Palmeiras), Thiago Silva (Chelsea), Alex Telles (Porto); Casemiro (Real Madrid), Philippe Coutinho (Barcelona), Fabinho (Liverpool), Bruno Guimaraes (Lyon), Douglas Luiz (Aston Villa), Everton Ribeiro (Flamengo); Everton (Benfica), Roberto Firmino (Liverpool), Gabriel Jesus (Manchester City), Neymar (Paris Saint-Germain), Richarlison (Everton), Rodrygo (Real Madrid).






## Messi ajumuishwa kikosi cha Argentina

**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi ameitwa kwenye kikosi cha awali cha Argentina cha wachezaji 30 kwa ajili ya mechi za mwezi ujao za kufuzu fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Ecuador na Bolivia.

Michuano ya kufuzu Kombe la Dunia kwa mwaka 2022 itakayofanyika Qatar ilitarajiwa kuanza Machi, lakini kutokana na mlipuko wa virusi vya corona ikasogezwa mbele hadi Oktoba, mwaka huu.

Sasa Argentina inayonolewa na Kocha, Lionel Scaloni ambayo haijashuka dimbani tangu Novemba, mwaka jana - itaanza kampeni yake dhidi ya Ecuador mjini Buenos Aires Oktoba 8, mwaka huu kabla ya kusafiri kwenda Bolivia siku tano baadaye.

Nahodha wa Argentina na Barcelona, Messi amejumuishwa kwenye kikosi cha awali pamoja na nyota wa Juventus, Paulo Dybala na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Wachezaji wawili ambao hawajawahi kuichezea Argentina, Facundo Medina na Nehuen Perez pia wamejumuishwa kwenye kikosi hicho, huku golikipa wa zamani wa Arsenal, Emiliano Martinez, anaweza kuanza kuichezea timu hiyo baada ya kukamilisha uhamisho wake wa kutua kule Aston Villa.

Kikosi kamili cha Argentina: Agustin Marchesin (Porto), Emiliano Martinez (Aston Villa), Juan Musso (Udinese); Marcos Acuna (Sevilla), Leonardo Balerdi (Marseille), Juan Foyth (Tottenham), Walter Kannemann (Gremio), Facundo Medina (Lens), Nicolas Otamendi (Manchester City), Nehuen Perez (Atletico Madrid), German Pezzella (Fiorentina), Renzo Saravia (Internacional), Nicolas Tagliafico (Ajax); Joaquin Correa (Lazio), Rodrigo De Paul (Udinese), Nicolas Dominguez (Stuttgart), Alejandro Gomez (Atalanta), Giovani Lo Celso (Tottenham), Alexis Mac Allister (Brighton and Hove Albion), Lucas Ocampos (Sevilla), Exequiel Palacios (Bayer Leverkusen), Leandro Paredes (Paris Saint-Germain), Guido Rodriguez (Real Betis); Lucas Alario (Bayer Leverkusen), Paulo Dybala (Juventus), Lautaro Martinez (Inter), Lionel Messi (Barcelona), Cristian Pavon (LA Galaxy) na Giovanni Simeone (Cagliari).

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PUMA YAMJAZA UTAJIRI NEYMAR

●●● Mkataba wake mpya na kampuni hiyo waweka rekodi mpya, unamfanya awapiku...

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI Mbrazil, Neymar, ameingia mkataba mnono na Kampuni ya Puma ambao utamwingizia kiasi cha pauni milioni 23 kwa mwaka ambao unatajwa udhamini huo ni mkubwa zaidi duniani kwenye michezo.

**Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, alimaliza mkataba wake na Kampuni ya Nike mapema mwezi huu, baada ya kuamua kuachana na kampuni hiyo ya Marekani ambayo alifanya nao kazi tangu akiwa na miaka 13.**

Mshambuliaji huyo wa PSG alikuwa amebakiza miaka miwili na Nike katika mkataba wake wa miaka 11, lakini alifikia uamuzi wa kuvunja mkataba na kujiunga na Puma baada ya kupewa ofa nono.

Inaelezwa mkataba huo mpya wa thamani ya pauni milioni 23, utamfanya Neymar kuingiza kiasi kikubwa cha fedha na kuwapita mastaa wenzake ambao ni Cristiano Ronaldo anayelipwa pauni milioni 15 na Nike ikiwa ni zaidi ya pauni milioni nane wakati Lionel Messi anapokea pauni milioni 18 kutoka katika Kampuni ya Adidas.

Kiasi kikubwa hicho cha fedha atakachopokea Neymar kimeweka hadharani na jarida ya Forbes, sambamba na The Sun, lakini bado haijajulikana muda wa mkataba ambao mchezaji huyo amesaini, huku Neymar tayari ameshaanza kuonekana akiwa kwenye matangazo na kampuni hiyo ya Ujerumani amevaa viatu na vifaa vya mazoezi.

Tangazo la Puma kuhusiana na mkataba huo limekuja na kauli mbiu isemayo 'Mfalme amerejea', ikikumbusha nembo ya kampuni hiyo ya 'Mfalme Puma'.

Neymar alisisitiza Puma wana historia na mchango muhimu ambao umesababisha mkataba wake na Nike kuvunjika.

'Nimekuwa nikiangalia picha za video za wachezaji wakongwe wa soka kama Pele, Cruyff, Matthaus, Eusebio na Maradona. "Ningependa kuona ninarejesha kumbukumbu ambayo iliwekwa na wanamichezo hao wakongwe uwanjani."

PSG inadhaminiwa na Nike na kampuni hiyo ya Marekani imesikitishwa na uamuzi huo uliofanywa na staa huyo, lakini klabu hiyo ya Paris bado inaamini Neymar atatekeleza majukumu yake vema kwenye timu.

Mbrazil huyo amethibitisha ataendelea kubakia Ufaransa msimu huu huku winga huyo akijipanga kufanya vema kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar aliisaidia PSG kucheza fainali ya michuano hiyo mwaka huu lakini bao 1-0 walilofungwa na Bayern Munich liliwapa vigogo hao wa Ujerumani taji hilo, huku klabu hiyo ya Ligue 1 ikionyesha kiwango cha chini.

## ZISIKUPITE

### UNITED, TELLES KIMEELEWEKA

MANCHESTER United imefikia makubaliano na mlinzi wa pembeni wa Porto, Alex Telles na nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 raia wa Brazil anaweza kusaini miaka mitano na klabu hiyo. ***(RMC Sport - via Mirror)***

### TOMORI ATAKIWA RENNES

KLABU ya Rennes imeitaka Chelsea kuwajumuisha wachezaji wawili katika mpango wao wa kutaka kumsajili golikipa, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 28 raia wa Senegal. Mlinzi wa England, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 22, ni mmoja wa wanaotakiwa na klabu hiyo ya Ufaransa. ***(Football Insider)***

### LIVERPOOL YAMTAKA DEMBELE

LIVERPOOL imeulizia uwezekano wa kumsajili kwa mkopo winga wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Barcelona, Ousmane Dembele, 23. ***(Sport)***

### BREWSTER KUTOLEWA MKOPO

KOCHA wa Sheffield United, Chris Wilder amefanya mazungumzo na Liverpool juu ya uwezekano wa kumchukua kwa mkopo straika, Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 20. ***(Yorkshire Live)***

### CITY YAMWANIA KOUNDE

MANCHESTER City inafikiria kumsajili mlinzi wa kati wa Sevilla, Jules Kounde, mwenye umri wa miaka 21 raia wa Ufaransa. Usajili huo unaweza kushuhudia Nicolas Otamendi, mwenye umri wa miaka 32, akienda upande mwingine. ***(Telegraph)***

### SORLOTH AWEKWA SOKONI

CRYSTAL Palace ina nafasi kubwa ya kumuuza straika wake, Alexander Sorloth mwenye umri wa miaka 24 raia wa Norway kwa RB Leipzig ili kupata fedha za kumsajili fowadi wa Brentford, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 25 raia wa Algeria. ***(Guardian)***

### RODRIGO ATAKIWA LEEDS

LEEDS United inaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa kimataifa wa Argentina, Rodrigo de Paul mwenye umri wa miaka 26 kutoka Udinese. ***(Fabrizio Romano)***

### JUVE KUMRUDISHA KEAN

JUVENTUS inawania kumsajili tena, Moise Kean, mwenye umri wa miaka 20 kutoka Everton baada ya raia huyo wa Italia kutokuwa na namba kwenye kikosi cha Goodison Park tangu alipotua kipindi cha majira ya joto mwaka 2019. ***(Goal)***

### YELDIN KUONDOKA NEWCASTLE

MLINZI wa kimataifa wa Marekani, DeAndre Yedlin mwenye umri wa miaka 27, anapanga kuondoka Newcastle United kwenda kujiunga na Besiktas. ***(NBC)***

### OLISE AGOMBEWA EPL

KLABU za Arsenal, Leeds United na Wolves zinawania kumsajili mlinzi wa Reading, Michael Olise mwenye umri wa miaka 18. ***(Football League World)***

### TRAORE AKARIBIA VILLA

ASTON Villa ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili winga wa kimataifa wa Burkina Faso, Bertrand Traore, 25, kutoka Lyon ya Ufaransa. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Mtibwa Sugar hesabu zitatimia

Na Shufaa Lyimo

BAADA ya kupata sare ya pili mfululizo, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema kikosi chake kitaendelea kucheza soka la ushindani ili kujiweka kwenye nafasi salama mapema tofauti na ilivyokuwa katika msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mtibwa Sugar ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu FC ya Mbeya, ikiwa ni wiki moja baada ya kupata matokeo hayo dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini, Dar es Salaam.

Katwila alisema kila mechi kwao ni muhimu na wachezaji wote wamejipanga kutorudia 'makosa' ya msimu uliopita.

Kocha huyo alisema ana uhakika msimu huu utakuwa wa kuvutia kutokana na kusajili wachezaji wenye uwezo na uzoefu wa kupambana kwa dakika zote 90.

"Naamini maingizo mapya ya wachezaji tuliowasajili yatatusaidia, msimu uliopita tuliponea chupuchupu kushuka daraja, lakini tulipambana mpaka tukabakia, hatutaki kurudia presha ile, "alisema Katwila.

Hata hivyo alisema anasikitishwa na baadhi ya mashabiki kuanza kuibeza timu kwa kushindwa kupata ushindi hali ya kuwa kila timu imejiimarisha kuvuna pointi.

"Nasikitika kuona kuna watu wanaibeza timu yangu, wanasema haina ubora, binafsi mimi naona timu yangu ipo vizuri na matunda yake watayaona, ligi ndiyo imeanza, tuwe na subira," Katwila alisema.

## Polisi Tanzania walilia uchovu

Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema uchovu waliokuwa nao wachezaji wake ndio sababu ya kushindwa kuondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa juzi mchana kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi mkaoni Kilimanjaro.

Mechi hiyo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1, wenyeji Polisi Tanzania wakitangulia kupata bao katika kipindi cha kwanza.

Malale alisema wachezaji wake hawakupata muda mzuri wa kupumzika na walishuka uwanjani huku miili yao ikiwa haijawa tayari kupambana.

"Uchovu ndio umesababisha tumepata matokeo haya, hata hivyo ninawapongeza wachezaji wangu kwa kiasi walichojituma, haikuwa malengo yetu kugawana pointi, tutaendelea kujipanga ili kuutumia vema uwanja wa nyumbani," Malale alisema.

Aliongeza kwa sasa wanaelekeza nguvu zao kwa ajili ya mechi inayofuata dhidi ya Dodoma Jiji FC, ambayo itachezwa Septemba 26, mwaka huu mkoani humo.

"Sasa hivi naiwazia mechi yetu na Dodoma Jiji FC lengo ni kupata pointi tatu katika mchezo huo ambao tunataka tuwape burudani mashabiki wetu," alisema kocha huyo.

# AZAM, MBEYA CITY HAPATOSHI SOKOINE

Na Saada Akida

WAKATI Azam FC inahitaji kuendeleza kasi ya ushindi, wenyeji Mbeya City wamepania kuanza vema katika mechi yake ya kwanza nyumbani ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema kikosi chake kiko katika hali nzuri na kimefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kupata ushindi katika mchezo huo wa raundi ya tatu.**

Vivier alisema kila mchezaji yuko tayari kupambana ili kupata pointi tatu muhimu na wataingia uwanjani kwa tahadhari.

"Tulifika salama na asubuhi ya leo (jana), wachezaji wamepumzika, jioni (jana jioni), ndio tutaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi iliyoko mbele yetu, tunajua mechi zote ni ngumu na tumejiandaa na hilo," alisema Vivier.

Kocha huyo aliongeza ushindani umeongezeka zaidi msimu huu, hivyo anawataka wachezaji wake kutumia vizuri nafasi za kufunga watakazozitengeneza.

"Tutamkosa Agrey (Morris), ila haitaathiri malengo yetu, tumekuja kutafuta alama muhimu katika mechi yetu hii, tunatambua wapinzani wetu nao wamejipanga kuhakikisha wanatumia vema uwanja wa nyumbani kwao," Vivier alisema.

Aliongeza baada ya kupata pointi sita nyumbani, sasa wanahitaji kupata ushindi ugenini ili malengo yao ya kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu yaendelee.

"Tumekuja huku kwa lengo la kutafuta matokeo chanya, tunahitaji kufanya vizuri katika mechi za ugenini kama tulivyokuwa nyumbani, hatutarajii kuacha pointi, tunahitaji kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa," alisema kocha huyo.

Naye Amri Said, Kocha Mkuu wa Mbeya City, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimeimarika na kinaamini leo wataondoka na ushindi.

"Tuliyafanyia kazi makosa yetu, tutaingia tofauti kama tulivyoonekana katika mechi dhidi ya Yanga, kila mechi kwetu ni muhimu, tumejifunza na tumejua tulipokosea," Said alisema.




Mgombea udiwani Kata ya Kivukoni jijini Dar es Salaam, Sharik Chouhule (katikati), akicheza muziki aina ya singeli wakati wa uzinduzi wa kampeni katika Kata ya Gerezani mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kiungo Azam mambo mazuri Israel*

Na Adam Fungamwango

KIUNGO wa Azam FC, Novatus Dismas, amevuka kiunzi cha kwanza, na sasa ameingia katika majaribio rasmi baada ya kufanya vema kwenye programu ya mafunzo ya awali katika klabu ya Maccabi Tel Aviv ya nchini Israel.

Ofisa Habari wa Azam, Thabit Zakaria, alisema kiungo huyo sasa amewekwa katika mpango wa majaribio kamili baada ya wakufunzi kuridhishwa na kiwango chake kwenye mechi ya kwanza ya majaribio aliyocheza akiwa na klabu hiyo.

"Mwanzo walipomchukua ilikuwa ni kwenda kwenye mafunzo, lakini baada ya mechi hiyo wametuambia wametoka kwenye mafunzo na sasa mchezaji wetu yupo kwenye majaribio kamili," alisema Zakaria.

Mchezaji bora huyo chupukizi wa msimu uliomalizika, ambaye alikuwa akiichezea Biashara United kwa mkopo yuko kwenye kikosi cha vijana chini ya umri wa miaka 20 (U-20).

Kiongozi huyo alisema kwa sasa ameingia kwenye majaribio ya siku 20, huku akitarajiwa kuongezewa mechi nyingine mbili kwa ajili ya kuangaliwa zaidi.

"Baada ya mechi hizo klabu hiyo itatoa ripoti kamili juu ya majaribio yake, lakini tunamatarajio makubwa atafanya vizuri," Zakaria alisema.

Maccabi Tel Aviv ni moja kati ya timu kubwa nchini Israel ambayo mara kwa mara huwa inashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa haifanyi vizuri sana kwenye mashindano hayo.

Azam ilimrejesha kiungo huyo msimu huu, baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia akiwa na Biashara United msimu uliopita.

# Michezo

Jumapili Septemba 20, 2020

Nipashe




Puma yamjaza utajiri Neymar UKURASA 22



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto' (kulia), akijaribu kumiliki mpira katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba jana. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Biashara hatumwi mtoto

**Na Somoe Ng'itu**

TUMEREJEA nyumbani! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United itakayochezwa leo kuanzia saa 1: 00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Hii ni mechi ya kwanza kwenye uwanja wa nyumbani kwa mabingwa hao watetezi ambao walianza msimu wa 2020/21 jijini, Mbeya dhidi ya timu mpya ya Ihefu FC na kupata ushindi wa mabao 2-1, halafu ikatoka sare ya goli 1-1 dhidi ya wenyeji Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro.

Sven aliliambia gazeti hili kikosi chake kimefanya vema maandalizi ya kuwakabili Biashara United kutoka Musoma, na anatarajia kutumia mfumo tofauti na mechi mbili zilizotangulia.

Kocha huyo alisema mechi zote ni ngumu na zina ushindani, lakini anapata matumaini ya kukusanya pointi tatu kutokana na kutumia uwanja wa nyumbani.

Naye Francis Baraza, Kocha Mkuu wa Biashara United, aliliambia gazeti hili wamekuja Dar es Salaam kutafuta matokeo mazuri na wanaamini watafanikiwa.

Baraza alisema 'ameisoma' Simba katika mechi zake zilizopita, hivyo anajua mahali 'atakapoizua' isifanye mashambulizi kwa timu yake.

"Tunajua tunakutana na mabingwa, wao wanataka pointi zitakazowaweka salama katika kutetea ubingwa na sisi tunataka ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri, malengo yetu ni kujihakikishia nafasi ya kubakia kwenye ligi hii," Mkenya huyo alisema.

# ZLATKO AMFUNIKA EYMAEL YANGA IKIOKOTA 3 KAGERA

## ●●● Sasa waongoza ligi wakati Kisinda, Mukoko waonana vyema wakimnyamazisha Maxime huku...

**Na Isaac Kijoti,** BUKOBA

YANGA gari limewaka! Ndivyo unavyoweza kusema kwa lugha nyepesi baada ya kuendeleza ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa jana katika Uwanja wa Kaitaba mjini hapa.

**Ushindi huo ni wa pili mfululizo baada ya mechi ya fungua msimu kulazimishwa sare dhidi ya Tanzania Prisons na kisha kuichapa Mbeya City bao 1-0, mechi hizo mbili zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.**

Lakini pia, kwa ushindi huo, unamfanya Kocha Mkuu wa Yanga, Mserbia Zlatko Krmpotic kufuta rekodi mbovu ya mtangulizi wake kuanza kwa kipigo dhidi ya Kagera Sugar.

Msimu uliopita, Januari 15, mwaka huu, Kocha Mbelgiji Luc Eymael, akiiongoza Yanga katika mechi yake ya kwanza alianza kwa kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Lakini pia ushindi huo ni mwendelezo wa Yanga kuichapa Kagera Sugar ikiwa nyumbani kutokana na raundi ya pili ya Ligi Kuu msimu uliopita kushinda goli 1-0 ikiwa hapa Kaitaba. Katika mchezo wa jana, Kagera Sugar ndiyo iliyoanza kuliandama lango la Yanga kwa kasi na ndani ya dakika 11 za awali ilipata kona mbili, lakini ilishindwa kuzitumia vema.

Hata hivyo, mfumo wa 4-4-2 unaotumiwa na Zlatko jana ulionekana kutokuwa rafiki sana kwa safu ya ushambuliaji iliyokuwa ikiongozwa na Michael Sarpong na Sogne Yacouba.

Tofauti na mechi zilizopita, jana Deus Kaseke alianzia benchi huku winga ya kulia, Tuisila Kisinda akilazimika kukimbia na mipira ndani badala ya kuimimina akitokea pembeni jambo ambalo Sarpong na Yacouba hawakuwa wakilishwa ipasavyo.

Hadi kipindi cha kwanza kinamalizika Yanga haikupata kona hata moja dhidi ya mbili za Kagera Sugar wakati timu zote zikipiga shuti moja moja lililolenga goli.

Kipindi cha pili kilianza kwa Kagera Sugar kuliandama lango la Yanga na kama Vitalis Mayanga angeongeza umakini angeweza kuwaliza vijana wa Zlatko dakika ya 47, lakini Kipa, Metacha Mnata alijaa vema langoni.

Dakika ya 56 Yanga ilifanya mabadiliko kwa kumtoa Kibwana Shomary na kumwingiza Kaseke huku Yacouba akimpisha Carlos Carlinhos. Kuingia kwa Carlinhos kuliifanya safu ya ushambuliaji ya Yanga kuwa na uhai na dakika mbili baadaye aliichangamsha kwa kupiga krosi mbili zilizochezwa na mabeki wa Kagera Sugar.

Dakika ya 71 Kisinda aliambaa na mpira wingi wa kulia na kujaa nao ndani ya 18 kabla ya kuachia krosi iliyomkuta, Tunombe Mukoko mahali pake na kuizamisha kimyani, hivyo kuiandikia Yanga bao la kuongoza.

Zlatko alifanya mabadiliko ya tatu dakika ya 83 kwa Haruna Niyonzima kuingia kuchukua nafasi ya Zawadi Mauya.

Niyonzima alizidi kuipa uhai zaidi safu ya ushambuliaji ya Yanga na dakika ya 88 Kisinda aliachia shuti kali lakini liliishia mikononi kwa kipa Chalamanda.

Hadi dakika 90 za mwamuzi, Hussein Athumani kutoka Katavi zinamalizika katika Uwanja wa Kaitaba jana, Yanga ilifanikiwa kuendelea kutangaza ubabe dhidi ya Kagera Sugar nyumbani kwa kushinda 1-0 kama msimu uliopita.

Katika mechi ya mapema jana mchana, Tanzania Prisons ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga. Kwa ushindi huo Yanga sasa imefikisha pointi saba na kupaa hadi kwenye uongozi wa ligi wakati Kagera Sugar yenye pointi moja imeshuka hadi katika nafasi ya 15.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >